# Kitabu cha Mwelekezo cha Wachungaji

## na

# Roho Mtakatifu

## Mwongozo kwa Wazee, Waalimu wa Biblia na Wanafunzi wa Neno la Mungu

***Kuhaririwa na Albert Fairweather***



***"Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"*** **Matendo ya Mitume 20:28**

Ukurasa wa nyuma

**Masomo kwenye Kitabu cha Mwongozo na Albert Fairweather**

Albert na Elaine Fairweather wamekuwa katika utumishi kwa ajili ya Bwana wakati wote kwa miaka mingi. Wanaishi Queensland, Australia. Albert amekuwa mtendaji katika upanzi wa kanisa Australia na Kenya. Amekua mhariri wa majarida la Kikristo kwa miaka mingi.
Hivi sasa mafundisho yake yanachapishwa kwa namna ya kitabu.



## Printing Aid Abroad

**Kitabu 1**

**Kitabu cha Maelekezo kwa Wachungaji na Roho Mtakatifu.**

Mwongozo kwa Wazee, Waalimu wa Biblia na Wanafunzi wa Neno la Mungu

**Kitabu 2**

**Mpango Mkuu wa Mungu wa Nyakati.**

**Masihi katika Unabii,**

**Kitabu 3**

**'Mambo Yajayo'**

**Mafunzo kuhusu vitabu vya unabii vya Danieli na Ufunuo wa Yohana**

**Hagai na Malaki**

**Kitabu 4**

**Ushindi dhidi ya Majaribu**

**Maisha na Nyakati za Ruthu**

**Kitabu cha Ayubu**

**Maisha na Nyakati za Ibrahimu**

**Maisha na Nyakati za Musa**

**Sauli na Daudi**

**Kitabu cha Yuda**

**Kupata Pumziko katika Majaribu**

Kunakili na kutafsiri sahihi vitabu hivi kwahimizwa.

**Vitabu vinachapishwa kadiri fedha inavyoruhusu, na vinapatikana katika muundo wa PDF kwa ombi.**

Ndani ya ukurasa wa kwanza **Tunayoamini**

## Twaamini katika:

[1] Biblia kuwa ni Neno la Mungu lenye uvuvio wake, ndiyo mamlaka kipekee ya mafundisho na utendaji.

[2] Utatu wa Mungu.

[3] Uungu na uanadamu usio na dhambi wa Bwana wetu Yesu Kristo.

[4] Utu na Uungu wa Roho Mtakatifu.

[5] Uumbaji na kuanguka kwa mwanadamu.

[6] Kifo cha Bwana wetu Yesu Kristo ikiwa sadaka ya dhambi za ulimwengu wote na ufufuo wake wa kimwili na kupaa kwake.

[7] Kurejea kwa Bwana wetu Yesu Kristo kimwili kabla ya milenia.

[8] Ufufuo wa mwili.

[9] Hukumu ya walio hai na waliokufa kwa Bwana Yesu Kristo.

[10] Ubarikiwa wa milele kwa wenye haki na adhabu ya milele kwa walio waovu.

[11] Uhalisia na utu wa shetani, aliyeumbwa na Mungu, lakini akaanguka kupitia kiburi.

[12] Umuhimu wa kuzaliwa upya ili kupata wokovu.

[13] Kudumisha matendo mema na maisha ya utauwa kwa wote wanaokiri kuwa Wakristo.

[14] Usalama wa milele wa muumini.

[15] Ubatizo kwa kuzamisha waumini wote.

[16] Kuwa Mitume na Manabii walikuwa kipindi cha msingi wa Kanisa na karama zao maalum za miujiza, uponyaji na ndimi hazipo tena nasi hivi sasa kwa kuwa tuna Maandiko yaliyo kamilika. Hata hivyo, twaamini kuwa ikiwa ni mapenzi ya Mungu, **Yeye** bado huponya kwa kuyajibu maombi.

[17] Wingi wa Wazee kama viongozi wa kiroho wa kanisa la mahali, wakisaidiwa na Mashemasi, bila kutawaliwa na baraza la nje.

[18] Kuadhimisha Chakula cha Bwana kila Jumapili, pamoja na mikutano ya maombi na mafundisho.

[19] Twaamini kujitawala kwa kila kanisa la mahali.

[20] Katika kanisa la mahali, wanaume na wanawake wana majukumu na utendaji kazi tofauti. Wanaume wanapaswa kutimiza majukumu ya uongozi na kuongoza katika mikutano yote ya hadhara na sala. Katika mikutano ya kanisa la mahali, wanaume wanapaswa kusali vichwa vyao vikiwa havijafunikwa, wanawake wakiwa wamevifunika vichwa vyao, kuashiria uongozi wa Kristo.

[21] Washirika wote wa mwili wa Kristo, Kanisa, wanapaswa kupokelewa hadi wakati ule watakapo ona hawawezi kuunga mkono mafundisho na mwenendo kama vile yalivyowekwa wazi katika Maandiko Matakatifu, Neno la Mungu.

## Yaliyomo

# Kitabu cha Mwelekezo cha Wachungaji

**Sura 1. Mchungaji Mwema**

**Sura 2. Kanisa ni nini?**

**Sura 3. Kanisa la Mahali**

**Sura 4. Majukumu ya Makanisa ya Mahali**

**Sura 5. Uongozi wa Makanisa ya Mahali**

**Sura 6. Uinjilisti na Upanzi wa Kanisa**

**Sura 7. Nyumba ya Mungu**

**Sura 8. Kuja kwa Bwana**

**Masomo ya Roho Mtakatifu**

Manukuu yote yametoka katika tafsiri ya Mfalme Yakobo (King James Version) ya Biblia Takatifu.

## Baadhi ya Sababu za Kitabu cha Mwelekezo

Kitabu hiki cha mwelekezo kimeandaliwa kama mwongozo wa Wazee, Waalimu wa Biblia na Wanafunzi wa Neno la Mungu wakitafuta kuongoza na kufunza makanisa ya mahali katika mfumo uliowekwa wazi katika Neno la Mungu. Kitakuwa cha msaada pia kwa Wakristo wapya na chaweza tumika katika vikundi vya Shule za Biblia na Madarasa pamoja na makanisa.

Katika masomo haya, tunawezakosa kufuata desturi na mafundisho ya madhehebu tofauti yaliyobuniwa katika karne zilizopita, lakini tutakua tukichunguza **kile ambacho Mitume walifundisha,** na kile ambacho **makanisa ya awali yalitenda** katika karne ya kwanza ya kipindi cha kanisa, kama vile iloivyonakiliwa katika Biblia.

**Usistaajabishwe na kile kinachofunzwa, bali uwe kama Waberoya walioyachunguza Maandiko kila siku na kuhakikisha kuwa yanalingana na Biblia (Matendo ya Mitume 17:10 - 12). Tafadhali soma kwa makini marejeleo yote ya Biblia**

***"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli"*** (2 Timotheo 2:15).

-----------------------------------------------------

# Umuhimu wa Neno la Mungu

**W**azee na Waalimu wa Biblia na waumini wote wanapaswa kuelewa kuwa Neno la Mungu linafaa **Kufunzwa** na **Kutiiwa** kwa uaminifu.

**M**arejeleo yafuatayo yanafundisha kuwa **Maandiko** yote:

- **Yamevuviwa na Mungu** (2 Timotheo 3:16-17)
- **Hayakuja kwa mapenzi ya mwanadamu** (2 Petro 1:19-21).
- **Yatadumu milele na hayatapita kamwe** (Mathayo 24:35).
- **Yana nguvu, hugawanya na kutambua** (Waebrania 4:12-13).
- **Ni ya muhimu kuliko chakula** (Mathayo 4:4).
- **Husafisha na kubadilisha maisha** (Zaburi 119:9; 1 Petro 2:1 - 3).
- **Hutakasa kimsimamo na kibinafsi** (Matendo ya Mitume 20:32; Wakolosai 3:16).

**Waumini wote wanapaswa kuwa na kicho kuelekea Biblia,** kwa kuwa ni Neno la Mungu lituongozalo katika maeneo yote ya maisha na imani yetu. Yatufunza njia ya kwenda mbinguni na jinsi ya kumpendeza Bwana. Mfalme Sauli aliupoteza ufalme na maisha yake kwa sababu alikataa kuelekezwa na Mungu na akakosa kulitii Neno la Bwana.

**S**amweli alimwambia Mfalme Sauli: *"Je! BWANA huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu, **Sawasawa na kutii sauti ya BWANA?** Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuiliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago. Kwa kuwa umelikataa neno la BWANA, Yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme"* (1 Samweli 15:22-23).

**N**eno la Mungu huwaandaa watu wote wa Mungu kwa ajili ya huduma zao maalum hivyo basi lapaswa kusomwa kwa makini (2 Timotheo 2:15; 2 Timotheo 3:16-17).

**T**afadhali ona maneno ya mwisho ya mtume Paulo kwa wazee wa kanisa la Efeso: *"Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa **neno la neema yake**, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa"* (Matendo ya Mitume 20:32).

**-----------------------------------------------------**

**Sura 1**

# Yesu akasema, 'Mimi ndimi Mchungaji mwema'

**Pia anaitwa 'Mchungaji Mkuu' na 'Mchungaji aliye Mkuu' anayejali nafsi zetu. Tunahitaji kuhakikisha kuwa ni Mchungaji wetu.**

**Y**esu akasema: *"Mimi ndimi Mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo"* (Yohana 10:11). 'Mwema' humaanisha 'halisi na kweli.' Yeye ni mwaminifu kwa Neno lake na anaweza tegemewa! Aliutoa *'Uhai wake kwa ajili ya kondoo'*. Wote wanao mwamini hupata msamaha, pumziko na amani mioyoni mwao katika safari ya maisha.

**K**atika Zaburi 23, Mfalme Daudi akasema: *"BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huniongoza. **Hunihuisha** nafsi yangu"*. Daudi alifurahia uhusiano na Bwana wake, kutafakari na kushirikiana naye. Akapata amani na pumziko la moyo ndani yake. Alifahamu hili: *"Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe upo pamoja nami."* Watakatifu katika karne nyingi zilizopita wamepata faraja katika Zaburi hii.

## Yesu alifunza mifano mingi

'Mfano' huonyesha ukweli wa kiroho kutokana na matukio ya kawaida kwao wanaosikiliza. Katika Luka Sura ya 15 kunayo mifano minne kama hii ya **vitu vilivyopotea,** na waliokuwa wakimsikiliza Yeye walikua watoza ushuru, wenye dhambi namna zote na Mafarisayo wa kidini zaidi!

**Ujumbe wake kuhusu kondoo aliyepotea.** Kondoo ni wapumbavu nao wana uzoefu wa kutangatanga. Mchungaji aliwaacha kondoo wake 99, na akamtafuta na kumpata kondoo aliyekuwa amepotea, akamweka mabegani na kumleta nyumbani. Akawaita majirani zake akawaambia, *"Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea!"* Yesu akaongeza: *"Nawaambia, vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu"* (Luka 15:1-7). Wakati mwingine tumetenda kipumbavu na kujiletea matatizo juu yetu na jamii zetu. Lakini Yesu ndiye 'Mchungaji mwema' anayewatafuta waliopotea kipumbavu.

**Ujumbe wake kuhusu sarafu iliyopotea.** Mwanamke alikua na shilingi kumi, akapotewa na moja. Sarafu ni kitu kilichokufa bila uwezo wa kujipata. Mwanamke akawasha taa, akafagia sakafu akitafuta. alipoipata aliwaita jirani zake pamoja akasema: *"Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimeipata tena shilingi ile iliyonipotea"*. Kwa hayo Yesu akaongeza, *"Vivyo hivyo kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye"* (Luka 15:8-10). Biblia yasema *"Nanyi **mlikuwa wafu** kwa sababu ya makosa na dhambi zenu, aliwahuisha"* (Waefeso 2:1). Kwa asili, tumepotea na wafu kiroho, lakini kwa kumwamini tunapokea maisha mapya katika Kristo, 'Mchungaji wetu mwema'.

**Ujumbe wake kuhusu mwana mpotevu.** Mtu mmoja alikua na wana wawili, yule mdogo akadai sehemu ya urithi wake **kabla** babake hajafa! Akaondoka nyumbani na akiwa nchi ya mbali akatapanya mali zake katika maisha ya uasherati. Ili aweze kuishi alipata kazi ya kuwalisha nguruwe, mnyama aliye najisi kwa Wayahudi. *"**Alipozingatia moyoni mwake**, alisema, ni watumishi*

*wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa! nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, "Baba, **nimekosa** juu ya mbingu na mbele yako, sistahili kuitwa mwana wako tena. **Nifanye** kama mmoja wa watumishi wako."* (Luka 15:11-24). Hii inaashiria toba ya kweli.

**B**abake alikua akimtazamia, na akamwona akiwa *'angali mbali'* akija. Akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana, akamvika na kumfanyia karamu, akasema, *'kwa kuwa huyu mwanangu **alikuwa amekufa**, na **amefufuka**; alikuwa **amepotea**, naye **ameonekana**. Wakaanza kushangilia.'* Yesu alifunua upendo wa Baba haata kwa wale waliokua wameyaharibu maisha yao kwa madawa ya kulevya, pombe na makahaba. Anaweza **fanya** jambo jipya na la kupendeza katika maisha yetu.

**Ujumbe wake kwa mwana mkubwa.** Ndugu mkubwa hakua na furaha aliposikia sauti ya nyimbo na machezo. Akamwambia baba yake, *"Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, **wala sijakosa amri** yako wakati wo wote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu. Lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona."* Huu ni mfano mzuri wa Mafarisayo waliokuwa na kiburi na wakidini sana, lakini Yesu alijaribu kuwapata hata wale ambao baadae watamsulubisha! *"Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa **amekufa**, naye **amefufuka,** alikuwa **amepotea,** naye **ameonekana**"* (Luka 15:25-32). Mungu anawapenda hata wenye dini waliopetea.

**B**aadhi yetu tumetenda dhambi zaidi ya wengine, lakini sio tu **kina** cha dhambi zetu, bali ni **uhakika** wa dhambi zetu. Biblia yasema *"kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"* (Warumi 3:23). Yesu akasema, *"Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja **kutafuta** na **kuokoa** kile **kilichopotea**"* (Luka 19:10). Kweli yeye ni 'Mchungaji mwema'.

**Msalabani, Bwana wetu alilipia adhabu ya kila dhambi iliyotendwa, ya wakati uliopita, uliopo, na ndio, wakati unaokuja! Na kutoka katika moyo wake wa upendo ulio mkuu, anatoa msamaha kamili na kipawa cha uzima wa milele kwa wote wanaotubu na kumjia.**

-----------------------------------------------------

**Sura 2**

# Kanisa ni Nini?

**Kanisa lilitajwa kwanza na Bwana wetu katika Mathayo 16:13 hadi 20.**

**N**eno la **'Kanisa'** ni neno **'Ekklesia'** katika Kigiriki na lamaanisha **'kikundi, kusanyiko ama umati wa walioitwa.'** Baadhi ya Wagiriki waliteuliwa ili kuunda 'Ekklesia' (Baraza teule) kusimamia mambo ya mji, naye Yesu angewaita kutoka kwa mataifa yote *'watu kwa jina Lake'*. Watu wake teule, kutoka kwa Wayahudi na Wayunani, ili waunde **Ekklesia au Kanisa Lake** (Matendo ya Mitume 15:14). Hilo ndilo **Kanisa la Ulimwengu wote,** linalojumlisha waumini wote, nalo **kanisa la mahali** ndipo waumini hukusanyika ili wamwabudu Bwana Yesu Kristo.

**Natumia herufi kubwa 'K' kwa Kanisa la Ulimwengu wote.** Neno **Ulimwengu wote** halipatikani katika Biblia, lakini nalitumia kueleza jinsi waumini wote **kutoka Pentekoste hadi wakati wa sasa,** wapo katika Kanisa, bila ya kujali madhehebu yao. **Kanisa la mahali katika somo hili litakua na herufi ndogo 'k' katika kanisa.** Hii itatusaidia kutofautisha kati ya hizo mbili. **Muktadha** katika Biblia zetu yatueleza ikiwa ni kusanyiko la mahali la kanisa ama ni Kanisa la Ulimwengu wote, mara nyingi huitwa *'kanisa la Mungu.'*

**K**anisa halipatikani katika Agano la Kale, kwa maana Paulo aliandika kwamba Mungu alimpa **ufunuo maalum: "***ya kwamba kwa **kufunuliwa** nalijulishwa siri hiyo (kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache, kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo), **siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine,** kama **walivyofunuliwa** mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika **Roho**"* (Waefeso 3:3-5).

## Roho Mtakatifu na Kanisa

**Y**esu aliwaambia wanafunzi wake kuwa baada ya kurejea mbinguni, atamwomba Baba amtume Roho Mtakatifu aje kukaa **'ndani'** ya wanafunzi Wake. Kabla ya haya alikuwa **'pamoja'** na wanafunzi wake (Soma Yohana 7:37-39; 14:15-18).

**K**wa kujibu ombi Lake, Baba alimtuma Roho Mtakatifu **katika siku ya Pentekoste, siku 50 baada ya Yesu kufufuka toka kaburini** (Matendo ya Mitume Sura ya 2). Huo ndio wakati Kanisa liliundwa, na tangu wakati huo wote wanaomwamini wanabatizwa na Roho Mtakatifu katika huu **mwili mmoja, Kanisa** (Soma 1 Wakorintho 12:13). Kanisa laitwa mwili, jengo na hekalu takaatifu ambapomwaumini wanajengwa pamoja kuwa maskani ya Roho Mtakatifu (Waefeso 2:19-22).

**T**unaliita Kanisa, kwa kuwa inajumlisha waumini wote, Wayahudi na Wayunani, kutoka ulimwenguni kote. Wengi wao wako mbinguni, na Yesu atakaporejea alivyoahidi atafanya (Yohana 14:1-3), atawachukua watu wake waliosalia duniani, Kanisa lake, hadi nyumbani mbinguni (1 Wathesalonike 4:13-18).

**P**entekoste yamaanisha 'ya Hamsini', na sikukuu hii ya Kiyahudi ya Agano la Kale iliadhimishwa siku 50 baada ya Kristo kufufuka kutoka kwa wafu. Jambo hili lilitimiiza Sikukuu hii aliyopewa Musa. Sikukuu hizi zote za Bwana zilitimizwa, au zitatimizwa na Bwana wetu Yesu Kristo. Soma kwa makini Mambo ya Walawi Sura ya 23.

## Yesu na Kanisa Lake

**Mathayo 16:13-16.** Bwana Yesu aliwauliza wanafunzi wake swali la muhimu zaidi kuwahi ulizwa: ***"Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"*** Wanafunzi wakawa na majibu tofauti, lakini Petro akawa na jibu sahihi: ***"Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai".*** Baba yetu wa mbinguni alimfunulia Petro hili, anavyofanya kwa wote wanaomwamini Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao kutoka dhambini (Mathayo 11:25-30).

**Mathayo 16:17-18.** Kisha Yesu akasema *"Wewe ndiwe **Petro*** (Kigiriki '**Petros',** ikimaanisha 'jiwe dogo'). *na juu ya **mwamba huu*** (Kigiriki **'Petra',** 'mwamba kuu wa msingi', Kristo Mwenyewe), ***nitalijenga kanisa langu"***. Ona maana tofauti ya jina **'Mwamba'.** Petro, jiwe dogo, na Yesu, mwamba mkuu wa msingi.

**B**wana Yesu Kristo ndiye 'Mwamba wa Zamani' ambapo tunapaswa kujenga nyumba zetu za uzima juu yake (1 Petro 2:6-8). Yesu akasema; *Basi **asikiaye** hayo maneno Yangu, **na kuyafanya,** atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake **juu ya mwamba"*** (Mathayo 7:21-29). Upepo wa maisha hauwezi kumtikisa Mkristo kutoka katika msingi huu.

**Mathayo 16:19.** Funguo hufungua milango, naye Petro alipewa funguo za kufungua milango ya wokovu kwanza kwa Wayahudi (Matendo ya Mitume Sura 2), pia kwa Wasamaria (Matendo ya Mitume Sura 8) na kisha kwa Mataifa (Matendo ya Mitume Sura 10).

**Mathayo 4:19. Petro alikua ameitwa amfuate Yesu,** kwa kuwa alimwambia, *"Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu"* (Mathayo 4:18). Tukiitikia mwito wake, ana mpango kwa ajili yetu, alivyokua nao kwa ajili ya Petro, naye atayafanya maisha yetu kuwa ya kufaa kwa Mungu, ikiwa tutatumia karama na vipawa ambavyo Mungu ametupa.

**Kuna vikundi vitatu vya wanadamu.** Biblia inasema, *"Msiwakoseshe **Wayahudi** wala **Wayunani** wala **kanisa la Mungu"*** (1 Wakorintho 10:32). Kanisa limeundwa na Wayahudi na Wayunani. Ikiwa wewe sio Myahudi, basi wewe ni Myunani, mmoja wa mataifa. Kanisa limejengwa juu ya Kristo, na sio juu ya Petro aliyemkana Bwana wake mara tatu na baadae kukemewa na Paulo (Wagalatia Sura 2).

**Petro hana funguo za mbinguni - Kristo ndiye aliye nazo!**

## Kanisa na Israeli

**K**anisa halipo chini ya Sheria ya Musa, kwa kuwa sheria ilipewa Israeli pekee. **K**anisa ni **kiumbe kipya** na chini ya **neema** (2 Wakorintho 5:17; Waefeso 2:8-10), *"Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa, neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo"* (Soma Yohana 1:15-18).

**K**anisa lilitajwa kwanza na Bwana Yesu katika Mathayo 16:13-19, na ilikua **katika wakati ujao** aliposema, ***"Nitalijenga kanisa langu".*** Hakusema ***"Nimekuwa nikilijenga Kanisa Langu".***

**K**anisa la kweli lilianza **Pentekoste,** siku 50 baada ya Kristo kufufuka kutoka kwa wafu (Matendo ya Mitume Sura 2), nalo litanyakuliwa, 'lichukuliwe' hadi mbinguni kumlaki Yesu mawinguni (1 Wathesalonike 4:13-18). Israeli watarejea katika nchi yao kwa kutomwamini, kama inavyotendeka hivi leo miaka 2000 baada ya kutawanyika kwa mataifa.

**B**aada ya Kanisa kunyakuliwa, 'dhiki kuu' itaanza, wakati wa *'taabu ya Yakobo'* (Yeremiah 30:7). Yakobo ni Israel. Wakati Isreali atakaponyenyekezwa, atamgeukia Bwana, na kurejeshwa kiroho, kama inavyofundishwa katika Zekaria Sura ya 12 hadi 14 na Warumi Sura ya 9 hadi 11 **.** Kitabu cha Isaya Sura ya 11 chatueleza kuhusu wakati ujao mkuu wa Israeli.

**Siku hizi Bwana anawachukua Wayahudi na Wayunani kuwa watu kwa jina lake ili kuunda Kanisa Lake.**

**T**aifa la Israeli liliahidiwa nchi ya Kanaani kama **urithi wa kidunia** ikiwa na masharti yaliyogetemea utiifu wao kwa Torati ya Musa. **Kanisa** lina **urithi wa mbinguni,** linalotegemea imani kwa Kristo pekee.

**T**ofauti na Israeli, Kanisa la Ulimwengu wote ni kiumbe kipya cha Mungu ambacho kiliundwa Pentekoste siku hamsini baada ya Kristo kufufuka (Matendo ya Mitume Sura ya 2) nacho kimepewa urithi wa kiroho katika Kristo mbinguni kwa neema na kutiishwa chini ya imani pekee (Waefeso 2:1-10; 1 Petro 1:1:3-5).

**Kanisa ni bibi arusi bikra na atakayekua mke** wa Kristo na pia **mwili** wa Kristo (2 Wakorintho 11:2; Ufunuo wa Yohana 19:19:6-8; Waefeso 1:22-23).

**Israeli ni mke mzinifu** wake Bwana, aliyetengwa kwa kukosa uaminifu, lakini atarejeshwa katika Ufalme wa Kristo unaokuja: *"Hakika kama vile **mke** amwachavyo **mumewe** kwa hiana, ndivyo mlivyonitenda mimi kwa hiana, **Ee nyumba ya Israeli,'** asema Bwana"* (Yeremia 3:20).

"*Kwa sababu Muumba wako ni **mume wako**, BWANA wa majeshi ndilo jina lake, na Mtakatifu wa Israeli ndiye Mkombozi wako; Yeye ataitwa Mungu wa dunia yote. Maana BWANA amekuita kama mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni, kama mke wakati wa ujana, atupwapo, asema Mungu wako. Kwa kitambo kidogo nimekuacha, lakini kwa rehema nyingi nitakukusanya. Kwa*

*ghadhabu ifurikayo nalikuficha uso wangu dakika moja, lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu, asema BWANA, Mkombozi wako. Kwa maana jambo hili limekuwa kama maji ya Nuhu kwangu; maana kama nilivyoapa ya kwamba maji ya Nuhu hayatapita juu ya dunia tena, kadhalika nimeapa ya kwamba sitakuonea hasira, wala kukukemea"* (Isaya 54:5-9).

**Kwa matukio ya mwisho yanayoelezea kuokolewa na kurejeshwa kwa Israeli kama watu na taifa, soma Zekaria Sura ya 12 hadi 14 na Warumi Sura ya 9 hadi 11.**

**--------------------------------------------------------**

**Sura 3**

# Kanisa la Mahali

**Kutajwa kwa pili kwa kanisa kwapatikana katika Mathayo 18:1-20**

**M**afundisho na utunzaji wa kundi katika makanisa ya mahali ni kazi hasa anayoipenda Bwana wetu Yesu Kristo ambaye aliwaamuru **wazee** wa Efeso kupitia kwa mtume Paulo: *"Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatiifu amewaweka ninyi kuwa* ***waangalizi ndani yake,*** *mpate* ***kulilisha*** *kanisa lake Mungu,* ***alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"*** Kwa haya mafundisho ya muhimu, soma Matendo ya Mitume 20:17-36.

**K**utunza kundi pia kuna thawabu maalum, kwa maana mtume Petro aliwaambia Wazee: *"Na Mchungaji mkuu aaaatakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka"* (Soma 1 Petro 5:1-5).

**Kanisa la mahali ni la kipekee:** Kila kanisa la mahali linapaswa kuwa **huru,** nalo litaajibika kwa Mungu pekee. Katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana Sura ya 1 Bwana Yesu aonekana akienda katikati ya vinara vinavyowakilisha yale makanisa saba yanayotajwa katika Sura za 2 na 3.

**Y**esu hakuliweka kanisa moja juu ya lingine; kila kanisa linawajibika kwa Bwana pekee. Kila kanisa la mahali linapaswa kuwa na azimio la kujitawala, kujitegemeza na kujizalisha.

**Kanisa la mahali sio jengo, lakini ni waumini wanaokutana katika jengo. Waumini wote ni washiriki wa Kanisa la kweli, mwili wa Kristo.**

## Ona alama hizi zote zinahusu kanisa la mahali.

**Katika Mathayo Sura ya 18 mstari wa 1 hadi 20** tunapata mafundisho Yesu aliyowapa wanafunzi kuwaandaa kwa ajili ya wakati makanisa ya mahali yatakapoundwa. Kwanza alitaja kanisa la mahali katika Mathayo 18:17. Kumbuka, kanisa lilikuwa katika wakati ujao kama vile alivyowafunza wanafunzi! Kitabu cha Matendo ya Mitume kinafunza kuwa watu walipokuwa wanaokolewa, **walikusanyika pamoja** katika makaniisa ya mahali (Matendo ya Mitume 2:42; 14:23). Waumini wote wanapaswa kutafuta kukusanyika pamoja na kanisa linaloamini Biblia. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kukusanyika **kwa jina Lake** (Mathayo 18:20).

1. **Mathayo 18:1-4. Washirika** wanapaswa kuwa **wameongoka.** Ni lazima tuje kwa Kristo kama watoto wadogo, tukijinyenyekeza, tukiziungama dhambi zetu na kumwamini Yesu kama Mwokozi kutoka kwa dhambi zote. Kuja kama watoto, Mungu anaanza kazi mpya ndani yetu na anaahiidi kuikamilisha (Wafilipi 1:6). Tuna mengi ya kujifunza , na pia kuziacha njia nyingi zetu za ulimwengu.
2. **Mathayo 18:5, 15-18. Kanisa linapaswa kuwapokea** katika ushirika wale **wote** ambao Bwana amewapokea. Lakini ni lazima **tuwakatae baadhi** ya wale **wanaosababisha migawanyiko** na kuwaweka mbali wanaoishi **maisha maovu** na hawatatubu. Ni kanisa la mahali linalopaswa kufanya hivi. (Soma Warumi 16:17-18; Tito 3:10-11; 1Wakorintho 5:1-5).
3. **Mathayo 18:6-14. Tunapaswa tusiwakwaze wala kuwadharau** au kuwakosesha wale walio wana Wake. Ni lazima tuishi maisha yanayompendeza Bwana mbele ya waumini na ulimwengu, tukitazama **maneno na mienendo** yetu, tusimpotoshe yeyote anayeyatazama maisha yetu. Kwa kuwa twasoma *"mpate kuyakubali yaliyo mema,ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo,"* (Wafilipi 1:10). Katika hili pia tunao mfano wa Bwana Yesu: *"Naye aliyenipeleka yu pamoja nami, hakuniacha peke yangu, kwa sababu nafanya sikuzote yale yampendezayo"* (Yohana 8:29).
4. **Mathayo 18:15-18. Kanisa la mahali lapaswa kuwa pahali** ambapo dhambi **haivumiliwi** na pia mafundisho ya Biblia yanafuatwa ili kukabiliana nayo; kwa sababu kanisa la mahali lina mamlaka ya **kutoa nidhamu** na lapaswa kufanya hivyo. Ndugu yetu akikosa, hatua ya kwanza ni kumwendea **peke yako** na kujaribu kumpata kutoka kwenye dhambi yake. Hatupaswi kueneza wazi dhambi yake. Baadaye, ikiwa hatasikia, chukua pamoja nawe mtu mmoja au wawili ili kumkabili katika upendo na njia ya kumjali. Katika haya yote ni lazima tukumbuke nasi pia tuna wepesi wa kutenda dhambi na ni lazima tutafute kumrejesha huyo ndugu (Wagalatia 6:1). Ikiwa amekataa kutubu, basi liambie kanisa ili washirika wote waamue. Tukiyatenda haya katika njia ya utauwa na kujali, jambo hili litafungwa na kutumiwa na kuungwa mkono na Bwana juu mbinguni.
5. **Mathayo 18:19. Kanisa la mahali** linapaswa kuwa pahali hapa duniani ambapo watu wote wanajifunza **'kukubaliana',** na neno hili linamaanisha **'kuwa na sauti moja'** kuwa na **'umoja'** kuenenda katika upendo na umoja, kisha Mungu atawabariki na maombi yatajibiwa (Soma Zaburi 133).

6. **Mathayo 18:20. Hii ndiyo namna ya chini zaidi ya kanisa la mahali:** Bwana wetu alisema: *"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao".* Hatukusanyiki kwa kiongozi

mwanadamu yeyote, mpangilio wa dhehebu au dini yoyote; tunakusanyika kwake Bwana wetu Yesu Kristo, kwa maana yeye ni Bwana wa wote.

## Sera za Mapokezi

**I**ngawa makanisa yanapaswa kuwapokea watu wa Bwana katika njia ya upendo na kuwajali (Warumi 14:1; 15:7), hawafai kuwa wazi kupokea mafundisho yoyote ya uongo au matatizo ambayo watu waweza leta. Ni jukumu la wazee na waalimu wa Biblia kufunza katika kanisa la mahali, nao wazee wanapaswa kukutana na wageni walio na imani tofauti kuwaonyesha mafundisho ya kweli (Tito 1:5-9).

**Biblia yafunza:**

- **a.** Tuwaangalie na kujiepusha na wale wanaosababisha migawanyiko na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho ya kweli (Warumi 16:17-18).
- **b.** Tuwaondoe katika ushirika wale walio wazinzi, walevi, n.k. (1 Wakorintho 5:9-13).
- **c.** Tusimame imara dhidi ya maadhimisho ya kisheria. Tuko chini ya neema, wala sio sheria ya Musa (Wagalatia 5:1-5).
- **d.** Tumkatae mtu aliye mzushi, baada ya kumwonya mara ya kwanza na ya pili, yaani mtu yeyote mwenye kushikilia maoni yake mwenyewe na hakubali kufunzwa au kurekebishwa. Yeye ni mwenye fitina asababishaye migawanyiko (Tito 3:10-11).

**N**eno la Mungu linafunza kuwa kanisa la mahali lina jukumu la kudumisha utaratibu mwema na kudumisha mafundisho ambayo mitume walifunza, na kuwakataa kwenye ushirika wale wanaoendeleza makosa au kuishi maisha ya uasherati.

**Tumeitwa katika uhuru,** uhuru wa kutenda kilicho **haki kulingana na Biblia.** Hata hivyo, hii sio **leseni** ya kutenda **tunavyopenda** kinyume na Neno la Mungu. Leseni ya dereva hutupa uhuru wa kuendesha gari, lakini sio ruhusa ya kuliendeshea gari upande usiofaa wa barabara na kuyahatarisha maisha yetu na ya maisha watu wengine! Kutotii Neno la Mungu sio ‘uhuru wa Kikristo.’

“***Basi, ndugu, simameni imara, mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu”*** (2 Wathesalonike 2:15).

**----------------------------------------------------------------**

### Sura 4

# Utendaji kazi wa Kanisa la Mahali

Kitabu cha Matendo ya Mitume chatupa **mifano** ya yale Wakristo wa kwanza na makanisa walifanya – **matendo yao!** Kitabu hiki kimeitwa ‘Matendo ya Roho Mtakatifu’.

Nyaraka za Paulo, Yakobo, Petro na Yohana zatoa mafundisho kwa makanisa ya mahali kuhusu yale wanapaswa kuamini na jinsi ya kuishi maisha matakatifu. Baada ya Roho Mtakatifu kupelekwa na Baba na Kanisa likaundwa (Matendo ya Mitume 2:1-4) kulikua na wanafunzi karibu 120 Yerusalemu! Petro alihubiri na 3,000 zaidi wakaongezwa (Matendo ya Mitume 2:40-41)

## Hii ndio mikutano ya makanisa ya mahali

**Hawa waumini wa kwanza** *“... wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali”* Ona mambo haya manne Wakristo wa kwanza Yerusalemu *“wakawa wakidumu”* katika **kutenda** (Matendo ya mitume 2:42).

**Walikutana pamoja:**

**1. Kwa ‘fundisho’ la mitume** (fundisho ni mafunzo). Kwa kifupi mitume walifundisha kile ambacho Bwana alikua amewafundisha (Matendo ya mitume 1:1-3) na kile aliochowadhihirishia baadae kupitia ufunuo. Kwa sasa haya yapatikana yameandikwa katika Agano Jipya na yapo hapo kwa ajili yetu kujifunza na kutii (Matendo ya Mitume 16:4-5).

**2. Kwa ‘Ushirika’.** Neno hili lamaanisha **‘kushiriki mambo yote pamoja’. Tunafurahia pamoja** mambo ya Bwana ambayo tunashiriki kupitia imani katika Yesu Kristo Bwana wetu. Pia tunahimizana na kusaidiana kila mmoja katika safari ya maisha. Tumeitwa katika ushirika huu na tunadumishwa ndani yake na Mungu mwenyewe (1 Wakorintho 1:9; 10:14-16; Waraka wa kwanza wa Yohana 1). Tunahitaji ‘ushirika’ wa upendo na kutunzana miongoni mwa watu wa Bwana.

**3. Kwa ‘Kumega mkate’.** Usiku ule Bwana wetu alisalitiwa, aliwaambia wanafunzi wake kutenda haya kwa ukumbusho wake kwa kushiriki katika **‘mkate na kikombe’** (Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-34). **Mkate** watukumbusha kuwa mwili wake ulioharibiwa kwa ajili yetu msalabani. **Kikombe chatukumbusha** kuwa alimwaga damu kwa ajili ya msamaha wa dhambi. Tumepata ukombozi kupitia damu yake (Waefeso 1:7).

Haya yalifanyika *“siku ya kwanza ya juma”,* siku ya ufufuo, Jumapili kwetu, wakati makanisa ya mahali yalikutana (Matendo ya Mitume 20:7; 1 Wakorintho 16:1-2). Mungu alianza uumbaji wake siku ya kwanza na ‘kuikamilisha’ siku ya sita. Wakati Bwana alipokufa, alisema *‘yote yamekwisha’* (Yohana 19:30). Akawa mle kaburini chini ya laana ya kuvunja Sheria siku ya Sabato (Jumamosi), bali alifufuka siku ya kwanza (Jumapili). **Wakristo ni kiumbe chake kipya** (2 Wakorintho 5:17) nasi tunapaswa kukutana siku ya kwanza ya juma ili tushiriki katika chakula cha Bwana.

**4. ‘Na kusali’.** Kanisa lilianza katika mkutano wa sala (Matendo ya Mitume 1:14; 2:1) na wakadumu katika kusali (Matendo ya Mitume 4:23-31; 12:12).

Wakati unaofaa unapaswa kutengwa kwa ajili ya kanisa kukutana wakati washirika waweza ombewa na pia kuombea mahitaji mengineyo.

**K**utoka katika **1 Timotheo 2:1-3** twajifunza kwamba *"kabla ya mambo yote"* ni agizo la mitume kwa makanisa yote ya mahali hivyo basi ni ya muhimu zaidi. **Vipengele mbalimbali vya maombi ni:**

**Dua** – Kwa nini tusali – pindi tunapokumbana na hitaji.

**Sala** – Ni nani tunayesali kwake – ni Mungu kwa kicho na imani.

**Maombezi** – Kuwaombea wengine – tunao uhuru wa kumfikia, ujasiri, uhusiano mtakatifu wa kumkaribia Baba wetu wa mbinguni na twaweza kumjulisha haja za mioyo yetu.

**Shukrani** – Sababu za kusali – matokeo kutoka kwa maombi yaliyojibiwa na mahitaji kutoshelezwa.

**Kwa ajili ya watu wote** – Ni nani tunayemwombea – wafalme na wananchi – bila upendeleo.

**Hii ni mikutano ya kanisa la mahali, nyakati za kufurahia ushirika pamoja.**

## Mikutano ya kanisa na majukumu ya wanaume na wanawake

**Kumega mkate au chakula cha Bwana:** Wakati Bwana alipoanzisha hicho Chakula, aliwaambia wanafunzi wake *"fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu"*. Alitumia '*mkate'* na *'uzao wa mzabibu'* wa watu ambao aliishi miongoni mwao (Marko 14:22-23).

**Divai:** Bila shaka yalikua maji ya mzabibu yaliyo chachuka kisha yakaongezwa maji kama wengi wanavyoamini desturi ya Wayahudi ilivyokuwa wakati huo. Makabila mengi yaliyo maskini na yenye kutengwa hayawezi kupata haya hivyo basi kinywaji mbadala kinachofaa lazima kipatikane. Waumini wengi hawawezi kunywa mvinyo ulio na kileo, na maji ya mzabibu hayapatikani. Chai ya rangi iliyotiwa sukari inapopoa yawezatumika.

**Mkate:** Haiwezekani kuutengeneza mkate kama ule Bwana wetu alioutumia; wakati huo waumini maskini wangetumia shayiri, na walio tajiri ngano kwa unga. Neno la Kigiriki linalotumika kwa *'mkate'*, uliotumika wakati wa 'Chakula cha Bwana' ni *'artos',* na linamaanisha *'mkate wa aina yoyote'* (W. E. Vine, Kamusi ya Ufafanuzi). Neno hili linarejelea **mkate kwa ujumla,** ulioundwa kutoka kwenye nafaka ya aina mbalimbali, kama ilivyotumika na watu ulimwenguni kote.

**W**aafrika hufanya mkate kutoka kwa unga wa mahindi, ilhali Waasia hutumia mchele. **Mungu huutazama moyo tunapokuwa tukimkumbuka.** Hakuna mazingaombwe katika mifano hii: ***"Mkate pekee na divai pekee, hata hivyo kwa imani ni ishara nzito, ya mbinguni na kiungu."***

**Ibada:** Kabla kumega mkate, tumia wakati kuliadhimisha jina la Bwana katika **kuabudu** kwa ajili ya ukuu wa utu wake, na kwa kumwimbia tenzi zinazofaa, kusoma na kutafakari vifungu vya Biblia vinavyotueleza kuhusu Bwana Yesu Kristo.

**M**moja wa **wandugu** anawezajiunga katika ibada, na sio tu wazee wa kanisa. **Kusanyiko lote** linahusika katika kumwabudu Mungu kwa nyimbo na kusema 'Amina'! Wanaume walio kanisani wana uhuru wa kuongoza kupitia sifa, shukrani, sala, tafakuri ama himizo kutoka katika Neno la Mungu inavyostahili kipindi hicho wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Kuongozwa na Roho Mtakatifu hakutangulii maandalizi ya kibinafsi. Kushiriki kwapaswa kuwa na utaratibu, kwa wakati, staha, heshima kwa Mungu na kuujenga mwili.

**N**dugu wa kiume wanapaswa kuongoza katika mikutano ya kanisa iliyo hapo juu; nao akina dada hawapaswi kuhusika katika sehemu ya hadhara. Kanuni zinazohusiana na haya zapatikana katika 1 Wakorintho Sura 11 hadi 14 na 1 Timotheo Sura 2.

## Mafundisho kuhusu Ukichwa

**K**wa karne zilizopita waumini wengi wamefuata mafundisho kuwa katika mikutano ya kanisa la mahali, wanaume wanapaswa kuwa na vichwa visivyofunikwa na wanawake wanapaswa kufunika vichwa. Haya yapo katika msingi wa 1 Wakorintho 11:1-22, na kuweka wazi:

**U**kichwa wa Baba na Kristo juu ya wanaume na wanawake; utaratibu wa asilia wa uumbaji wa mwanamume kwanza, kisha mwanamke; Ambao malaika ni watazamaji wa makanisa ya mahali yanayoonyesha utaratibu na uongozi, na ilikua *'desturi',* au *'matumizi ya kidesturi'* ama *'mazoea'* ya makanisa yote siku za Paulo.

**Ona haswa maneno ya Paulo:** *"Basi, nawasihi mnifuate mimi. Kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu, aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana,* ***atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa****"* (1 Wakorintho 4:16-17).

**Muktadha ni kusanyiko la kanisa:**

"*Basi* ***mkutanikapo pamoja*** *haiwezekani kula chakula cha Bwana. Kwa maana kila mmoja hutangulia kutwaa chakula chake katika kule kula; hata huyu ana njaa, na huyu amelewa"* (1 Wakorintho 11:20-21)

**K**orintho ulikua ni mji wa bandari, wenye mchanganyiko wa tamaduni mbalimbali. Kile ambacho Paulo alifundisha hapa alifundisha makanisa mengine yote, nayo hayakuwa yanahusiana na **tamaduni ya Korintho,** bali mambo yote yalihusiana na **utaratibu alioutoa Mungu.** Hata ilitofautiana na desturi za Kiyahudi, ambapo hata leo wanaume hufunika vichwa vyao na wanawake huvifunua vichwa vyao katika ibada za masinagogi.

**M**anyumbani na makanisani, wanaume na wanawake wana 'majukumu' yanayotofautiana. Hata hivyo, wanawake sio duni wanapolinganishwa na wanaume, kwa maana ninyi nyote mmekuwa "mmoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:28). Wanawake pia wana karama na huduma maalum, haswa kufundisha wanawake wengine na watoto na katika ushuhuda wao nje ya mikutano ya kanisa (Tito 2:1-5; Wafilipi 4:3).

**D**ebora alitoa unabii akiwa ameketi chini ya mtende, wala sio katika Hema ya kukutania (Waamuzi 4:4-5) na binti wanne wa Filipo walitoa unabii, wala sio katika mikutano ya kanisa (Matendo ya Mitume 21:8-9). Biblia haijipingi yenyewe.

**I**ngawa mwanamume ni kichwa cha mkewe, naye mke anapaswa kumtii mumewe, mume anapaswa ampende mkewe kama vile Kristo alivyolipenda kanisa (Waefeso 5:22-33). Anapaswa kutafuta njia ya kumjenga katika imani na kuhakikisha kuwa amefikia uwezo wake wote kama mke na mama, akimhimiza kutumia na kukuza karama zake maalum kwa sababu yeye pia ni sehemu ya mwili wake Kristo, Kanisa.

**N**yumba ya Mkristo inapaswa kuwa mahali pa upendo wa Kikristo na umoja, kielelezo kwa wasioamini walio karibu. Katika tamaduni zingine, waume huwapiga wake zao, lakini hili halipaswi kutendeka katika nyumba ya Mkristo. Prisila alimsaidia mumewe Akila katika kumfundisha Apolo, na walitumia nyumba yao kwa ajili ya mikutano ya kanisa jipya (Matendo ya Mitume 18:1-26, 1 Wakorintho 16:19).

**M**adirisha ya kanisa yanawezafunguliwa kupokea upepo wa mabadiliko ya kitamaduni na hekima itokayo kwa mtizamo wa ulimwengu. Wazee wa kanisa wanapaswa kukataa mabadiliko yanayopingana na mafundisho ya kibiblia.

**Sheria zinaundwa katika mataifa mengi kuhalalisha kille ambacho Mungu ametukataza. Mungu atawahukumu wanaotenda mambo hayo.**

------------------------------------------------------

**Sura 5**

# Uongozi wa Makanisa ya Mahali

**U**taona katika funzo hili tunatumia neno 'Mzee', 'Mwangalizi', 'Shemasi' na 'Waalimu' kwa maana haya ndio maneno Biblia inayatumia kwa viongozi, wachungaji na watumishi wa makanisa. Hatutumii 'Askofu', 'Padre' 'Baba' 'Kasisi' ama 'Mchungaji', kwa maana haya ni majina ya vyeo ambavyo vimewaweka wanadamu kuwa juu ya makanisa.

**K**atika mafunzo haya, tutaangalia kile **ambacho mitume walifunza, kama ilivyonakiliwa katika Biblia zetu**, na kile **ambacho makanisa ya kwanza yalifanya** katika karne ya kwanza enzi ya kanisa, na sio desturi na mafundisho ya madhehebu mbalimbali zilizoundwa kwa karne nyingi.

**Nimethibitisha katika upanzi wa kanisa Australia na Afrika Mashariki kuwa tunawezarejea kwa kile kilichokua desturi ya kanisa la kwanza nayo yafanya kazi. Njia za Mungu ni bora kuliko zile zilizobuniwa na wanadamu.**

## Kwanza, Mitume

**Ona jinsi tunavyowatambua mitume wa kweli na walio waongo. Neno Mitume lamaanisha 'aliyetumwa'. Walikua:**

1. **Walichaguliwa na kuteuliwa** na Bwana – Marko 3:13-19.

2. **Waliitwa** 'mitume' Bwana – Luka 6:12-16.

3. **Walitumwa** na Bwana ili wamshuhudie Bwana – Yohana 15:26-27.

4. **Walikuwa pamoja naye** tokea **ubatizo wa Yohana hadi kupaa kwake** – Matendo ya Mitume 1:21-26.

5. **'Walimwona'** Bwana – 1 Wakorintho 9:1.

6. Walipewa uwezo wa kufanya **ishara na maajabu** kuthibitisha utume wao – Matendo ya Mitume 5:12.

**M**itume wote **walimjua na 'kumwona' Bwana,** isipokuwa Paulo, **'aliyemwona'** Bwana wakati wa kuongoka kwake, '*kama mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake'* (1 Wakorintho 15:8; Matendo ya Mitume Sura 9).

**H**akuna mtu yeyote leo **'amemwona Bwana'** na anaweza dai kuwa ni 'mtume'. Biblia inasema; *"Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo"* (2 Wakorintho 11:13-15).

**M**itume waliuweka msingi wa Kanisa kwa **jinsi walivyoishi** (Matendo ya Mitume 20:17-30); na kwa **kile walichofundisha** (1 Wakorintho Sura 3). Kile walichofunza kinaitwa **fundisho la mitume (mafunzo):** *"Wakawa wakidumu katika **fundisho la mitume,** na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali"* (Matendo ya Mitume 2:42); *"Basi walipokuwa wakipita kati ya miji ile, wakawapa zile amri zilizoamriwa na mitume na wazee walioko Yerusalemu, ili wazishike"* (Matendo ya Mitume 16:4). Haya yamenakiliwa katika Biblia zetu, Neno la Mungu lililovuviwa.

## Kuuweka Msingi

**Mitume** na **manabii** ni wa **kipindi cha msingi wa Kanisa. Walifundishwa na Bwana,** na baada ya kupaa kwake **wakapokea ufunuo** kutoka kwa Bwana ili wakamilishe mafundisho (1 Wakorintho 3:9-23; Waefeso 2:19-21).

**Wao na karama zao maalum za miujiza, uponyaji na ndimi hazipo pamoja nasi, kwa kuwa tuna Maandiko yaliyokamilika.**

**T**afadhali angalia 1 Wakorintho 13:8-13: Ile iliyo **'kamili'** (Kigiriki ni hali huru katika jinsia) ijapo, iliyo **'kamili'** na **'kamilika'** Neno la Mungu. **'Kamili' sio 'mtu', ni 'jambo' fulani.** Maandiko pekee ndio 'kitu' kilicho **'kamili'** ulimwenguni hivi leo (**'kamili'** yamaanisha **'kamilika'**). Maandiko **'kamili'** yaliyokamilika ndio **mtazamo wa karibu**; **mtazamo wa mbali** utakua wakati ufalme wake **'mkamilifu'** utakapoanzishwa duniani.

**K**arama hizi hazihitajiki leo ili kuwe na utendaji kazi wa kawaida katika kanisa la mahali. Zilikuwa ni za **muda mfupi** kiasili, na zilitumika na Mungu kimsingi kwa kusudi la **kuhakikisha** na **kudhibitisha** ujumbe wa mitume. Zilikuwa zimezuiliwa kabisa kwa matumizi yake katika 1 Wakorintho Sura 14. Hata hivyo, tunaamini kuwa miujiza na uponyaji hutendeka leo kwa kuyajibu maombi na kama impendezavyo Bwana.

**M**itume waliwateua wazee katika makanisa yote ili waendeleze kazi yao. Timotheo na Tito waliagizwa wahakikishe wazee wameteuliwa katika makanisa. Waumini walipaswa kuwatambua na kuwaheshimu wazee zaidi katika upendo (1 Wathesalonike 5:12-13). Pia walipaswa **kuwatii** (1 Petro 5:5).

**Mitume waliwapokeza 'wazee' fimbo. Tumeagizwa kuwateuwa wazee katika makanisa, wala sio mitume –** Matendo ya Mitume 14:23.

## Pili, Manabii

**U**nabii ulikuja kupitia manabii waliokuwa wamekirimiwa. Unabii ni tangazo la kile kisichoweza kujulikana kwa njia ya kawaida. Kulikuwemo maonyo kuhusu matukio yajayo na ufunuo wa mafundisho. Kusudi lake lilikuwa ni kuelimisha (kujenga), kuhimiza (kuchochea) na kufariji (kuponya) waumini (1 Wakorintho 14:1-3).

**M**anabii walitoa jumbe zilizovuviwa kutoka kwa Mungu makanisani kwa sababu waumini hawakuwa na Biblia. Vyuo vya vitabu vya Agano la Kale vilikua nadra, ghali na vikubwa navyo vilikua vichache. Vitabu vya kwanza vya Agano Jipya havikuandikwa kwa miaka kadhaa hadi baada ya kufufuka na kupaa kwa Kristo.

**K**itabu cha Ufunuo kilichoandikwa na Yohana takriban 96BK kilikamilisha kanoni ya Maandiko. Chochote hakifai kuongezwa kwa ufunuo uliokamilika katika Biblia zetu (Ufunuo 22:18-19; Yuda 3). **Biblia kama vile tunavyoijua ilikuja baadae.**

**Leo wazee na waalimu wamechukua nafasi ya mitume na manabii, nao hulijenga, kuhimiza na kufariji wanapokusanya na kufunua hazina katika Maandiko yaliyokamilika.**

## Tatu, Wachungaji ambao ni Wazee

**N**eno lililotafsiriwa kama 'mchungaji' katika Biblia linapaswa kuwa 'mchunga mifugo', linalotafsiriwa kutoka kwa neno la Kigiriki 'poimainō'. Wazee ndio wachungaji, na kila kanisa linapokua linapaswa kuwa na idadi ya wazee ambao pia ni waalimu. *"Pasipo mashauri taifa huanguka; bali kwa wingi wa washauri huja wokovu"* (Mithali 11:14).

**P**aulo aliwaita **wazee** wa kanisa la Efeso wakutane naye Mileto (sio Mchungaji, Mhudumu au Askofu, Matendo ya Mitume 20:17; Wafilipi 1:1). Akawaeleza hawa **wazee**, *"Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, mbalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa **waangalizi** ndani yake, mpate **kulilisha** kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"* (Matendo ya Mitume 20:28). Sufa za kustahili na utumishi wa Wazee

**Neno 'mzee'** laelezea yule aliye **komaa kiroho**, na '**kazi'** ya wazee ni **'kusimamia'** na **'kuchunga'** kundi. **Haya ni maneno ya 'kufanya' na 'kujali' wala sio majina ya kutwaliwa kama beji ya mamlaka.** Neno la Kigiriki la **'mchunga mifugo'** limetafsiriwa kama **'mchungaji'** ilhali neno **'msimamizi'** limetafsiriwa **'askofu'** katika kafsiri za kale za Biblia.

Hivi sasa maneno haya yanatumika kama **mataji ya viongozi wa kanisa**, lakini hili **halina mamlaka** kutoka kwa Neno la Mungu kufanya hivyo. *"Akaketi chini (Yesu), akawaita wale Thenashara akawaambia, "Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote"* (Marko 9:35).

## Heshima na Jukumu la Wazee

**N**eno **'mzee'** linadokeza **heshima** ya ofisi.

**M**aneno **'msimamizi'** na **'mchungaji'** yanadokeza **majukumu** ya ofisi.

**Majukumu** ya wazee ni **'kusimamia'** na **'kulichunga'** kundi.

**Kusimamia** ni mtazamo wa mbali, kwa kuwa inamaanisha **'kusimama mahali mashuhuri'** na **'kuliangalia'** kundi, kutafuta malisho mazuri, maji na hatari kutoka kwa wanyama pori. **Wazee** wanafaa kulilinda kundi kutokana na hatari.

'**Kulichunga'** (kitenzi) ni mtazamo wa karibu na inamaanisha *'kulilisha kundi kwa Neno la Mungu na pia matendo mengine ya kutunza maalum'.* Petro anatumia maneno mengine katika 1 Petro 5:1-5 yaliyo sawa na ya Paulo katika Matendo ya Mitume 20:28. Zaburi 23 zamdhihirisha 'Mchungaji mwema' akiwatunza kondoo Wake.

**N**eno **'mchungaji'** limetolewa kutoka Waefeso 4:11 na halipaswi kutafsiriwa **'mchunga mifugo'**. Neno 'Mchungaji' limepewa maana zaidi ya kile Biblia yafunza na mara kwa mara limemweka mwanadamu **juu** ya waumini wenzake. Wazee ndio 'wachungaji' **'miongoni mwa kundi'** na huongoza kwa kuwa **kielelezo.** Petro aandika:

"*Nawasihi **wazee walio kwenu,** mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye: **Lichungeni** kundi la Mungu lililo kwenu, na **kulisimamia,** si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa **kutaka fedha ya aibu,** bali kwa*

*moyo. Walaa si kama wajifanyao **mabwana** juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya **vielelezo** kwa lile kundi"* (1 Petro 5:1-3).

**M**aneno haya hayakukusudiwa kutumiwa kama mataji au beji za kujitofautisha. Bwana Yesu alituonya dhidi ya haya katika Mathayo 23:1-12: *"Bali ninyi msiitwe **'Rabi'**; maana **Mwalimu** wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu **baba** duniani; maana **Baba** yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe **viongozi;** maana **Kiongozi** wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu. Na ye yote atakayejikweza, atadhiliwa; na ye yoteatakayejidhili, atakwezwa."*

**W**azee huongoza kwa kuwa vielelezo wala sio kwa mabavu. Kwa njia hii wanapata heshima kutoka kwa kundi ambao wanafaa kuwastahi sana katika upendo kwa ajili ya kazi zao na kuwatii (1 Wathesalonike 5:12-13; Waebrania 13:7, 17).

**Mzee ni yule aliyekomaa kiroho, karama na kazi yake ni kufunza, kusimamia na kulichunga kundi.**

## Umuhimu wa usimamizi unaotenda kazi

**Idadi** ya wazee **inayofaa** kwa **kulitunza** kanisa la mahali ni **watatu ama zaidi.** Biblia yaita hili **'usimamizi'** (1 Timotheo 3:1-2). Wazee wanapaswa kukutana mara kwa mara na kumgoja Bwana awape mwelekeo katika mambo yote yanayohusu kundi. Mzee mmoja hafai kuwatawala wazee wenzake, bali wote wanafaa kukutana kwa unyenyekevu wakiwadhania wengine kuwa bora kuwaliko. Kanisa la mahali ni la Theokrasia naye Bwana akiwa ndiye kichwa.

**1.** Ili kuwe na uongozi wa kibiblia, ni lazima kuwe na watu wa kiroho wanaojua Biblia zao, na ambao wana uzoefu wa kukuza na kutumia karama zao.

**2.** Kumtegemea mtu yeyote mmoja katika uongozi yaweza zuia ukuzaji wa karama, kuzuia upanzi wa kanisa na kutumia fedha katika kutimiza mahitaji ya mchungaji.

**3.** Idadi ya wazee inapelekea kushiriki mzigo wa kulitunza kundi walilokabidhiwa. Jambo hili pia lasawazisha utu kulingana na nguvu na udhaifu wao.

Wazee wanapomgojea Bwana kwa maombi, mapenzi Yake yataafikiwa.

"***Kwa maana mlikuwa mnapotea kama kondoo, lakini sasa mmemrudia Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu"*** (1 Petro 2:25).

## Msaada wa kifedha wa Wazee

**K**wa sehemu kubwa, wazee **hujitegemeza kifedha,** isipokua kwa wale ambao *'hujitaabisha kwa kuhutubu na kufundisha'* - yaani, wale wazee waliotoa muda wao wote kutunza na kufunza kundi. Hao *'wahesabiwe kustahili heshima maradufu'* na wanapaswa kusaidiwa na vipawa kutoka kwa makanisa na waumini (1 Timotheo 5:17-18).

## Mashemasi

**Mashemasi** (humaanisha 'watumishi') huwasaidia wazee katika kazi ya kanisa la mahali. Sifa za ustahili za wazee na mashemasi zapatikana katika 1 Timotheo Sura 3 na Tito Sura 1. Ni lazima wawe na ushuhuda mzuri katika jamii na kanisani, wawe na tabia nzuri, wawe na mke mmoja pekee. Wake za wazee na mashemasi yafaa wawe wanawake watauwa wenye busara.

**Mashemasi huwasaidia wazee katika shughuli mbali mbali za kanisa.**

## Nne, Waalimu

**L**eo hii, waalimu stadi hukusanya na kuvuna kutoka katika Neno la Mungu. Mwalimu mwenye kipawa humngojea Mungu akilitafakari Neno la Mungu. Roho wa Mungu humshawishi moyoni mwake yale Maandiko atakayosoma na ni kipi atakachofundisha kundi.

**W**aalimu wamechukua nafasi ya manabii. Wazee nao pia wanafaa wawe na uwezo wa kufunza: *"Basi imempasa **askofu (mzee)** awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, **ajuaye kufundisha**; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu, bali awe mpole, si mtu wa kujadiliana wala **asiwe mwenye kupenda fedha**"* (1 Tim. 3:2-3)

## Uwazi na Uajibikaji

**Biblia yatoa onyo kali kuhusu fedha:** *"Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha, ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani na kujichoma kwa maumivu mengi"* (1 Timotheo 6:10).

**Fedha zaweza kuwa majaribu:** Baadhi ya watu waweza kutamani na kuzitumia vibaya au hata kuiba fedha za kanisa. Matoleo yote yanapaswa kuhesabiwa na **wazee au mashemasi wawili au zaidi,** na kuhifadhiwa salama kwenye benki pamoja na **masimulizi mazuri ya uhasibu yaliyohifadhiwa na kusainiwa.** Wazee na mashemasi wanafaa kukutana na kuamua ni sehemu ipi katika kazi ya Bwana inapaswa kupokea msaada.

**U**angalifu mkuu unapaswa kuchukuliwa kuhusiana na matoleo ya watu wa Bwana kwa sababu zimetolewa kwa Bwana.

**P**aulo aliandika haya kuhusu kipawa kilichotolewa na makanisa ili kipelekwe kwa waumini maskini walioko Yerusalemu: *"**tukijiepusha na neno hili:** mtu asije akatulaumu kwa habari ya karama tunayoitumikia; **tukitangulia kufikiri yaliyo mema, si mbele za Bwana tu, ila na mbele ya wnadamu.** Nasi pamoja nao tumemtuma ndugu yetu tuliyemwona mara nyingi katika mambo mengi kuwa ana bidii, na sasa ana bidii zaidi sana kwa sababu ya tumaini kuu alilo nalo kwenu"* (2 Wakorintho 8:20-22).

**Wazee na waalimu wanapaswa kuwafundisha washirika wa kanisa kuhusu unyofu katika sehemu zote za maisha yao.**

----------------------------------------------------

**Sura 6**

# Uinjilisti na Upanzi wa Kanisa

**K**abla ya Bwana Yesu Kristo kurejea mbinguni, aliwaamuru wanafunzi wake akawaambia: *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, **mkawafanye** mataifa yote kuwa **wanafunzi**, **mkiwabatiza** kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na **kuwafundisha** kuyashika **yote** niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi **nipo pamoja nanyi** siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Amina* (Mathayo 28:18-20). Jambo hili laitwa **'Utume Mkuu'.**

## Kuwafanya Wanafunzi

**K**itabu cha Matendo ya Mitume kinanakili kwamba Petro, Yohana, Stefano, Filipo, Barnaba, Paulo na wengine wengi walihubiri injili, wakiwaeleza wengine kuhusu Bwana. Wengi waliongoka na makanisa mapya yakapandwa. Hii inapaswa kuwa kigezo chetu cha kufuata hivi leo.

**K**uwafanya wanafunzi yamaanisha kuwafunza waumini wapya siyo tu baadhi ya mambo, bali **'mambo yote'** yanayopatikana katika Neno la Mungu. Mwanafunzi ni **'yule mwenye nidhamu'** anayejifunza kumfuata Bwana na anafuata ili ajifunze.

**M**wanafunzi ana **'usadikisho'** kuhusu mafundisho ya kweli ya Neno la Mungu naye hataondoka na kuyaacha. Mwanafunzi huwa **'anajitolea'** kwa Bwana na njia zake jinsi zinavyodhihirishwa katika Neno la Mungu, na pia anajitolea katika kanisa la mahali na majukumu yake.

## Ni lazima wanafunzi waishi maisha yaliyotakaswa

**I**kiwa Bwana atatutumia, ni lazima tuishi maisha yaliyotakaswa. Neno **'kutakaswa'** lamaanisha **'kutengwa kwa ajili ya kazi ya Mungu'.** Kutengwa mbali na dhambi na kujitumikia mwenyewe. Wanafunzi wanapaswa:

**1.** Kufanya **usomaji** na **kulitafakari** Neno la Mungu kuwa mazoea ya kila siku. Hii yamaanisha kuutumia muda kuwaza kuhusu kila msitari na kuutumia maishani mwetu.

**2.** Kumbuka **nafasi** yako katika Kristo. *"Kwa maana **mlikufa,** na **uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.**Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai weyu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu"* (Wakolosai 3:3-4). Kristo alipokufa, ulikufa naye, kisha ukafufuka naye.

**J**ambo hili lilikuwa ni muhimu kwake Paulo: *"**Nimesulubiwa pamoja na Kristo**; lakini ni hai, wala si mimi tena, bali **Kristo yu hai ndani yangu**; na uhai nilio nao sasa katika mwili, **ninao katika imani ya Mwana wa Mungu**, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu"* (Wagalatia 2:20). **A**liyafunza haya kwa makanisa: *"Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwak, mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena"* (Warumi 6:5-6).

## Kuenenda katika nuru – Kuwafundisha wanafunzi haya

**1. Hali yako i vipi mbele ya Kristo?** Unapotenda dhambi, soma 1 Yohana Sura 1. *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote"* (1 Yohana 1:9). Damu ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu **hutusafisha** (yaendelea kutusafisha) dhambi yote. Pindi unapoungama dhambi yoyote, inuka baada ya kupiga magoti na uendelee kumtumikia Mungu kwa kuwa amekusamehe na akasahau.

**2. Wakristo wote hutenda dhambi nyakati nyingine.** Sisi sio wakamilifu. Usiruhusu **dhamiri inayokushtaki** ikusumbue, kwa kuwa umesamehewa. Ibilisi anataka akuweke chini uso wako ukiwa katika tope na mguu wake ukiwa kwenye shingo yako! Msihi Bwana akupe neema ili uenende katika unyenyekevu mbele zake na kushinda kila jaribu.

**3. Jifunze kuenenda kwa imani, wala sio kwa hisia.** Kuenenda katika nuru yamaanisha hamna dhambi inayojulikana kati yako na Bwana. *"Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli. Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote"* (1 Yohana 1:6-7).

**U**kisimama chini ya nuru, hakuwi na kivuli. Ikiwa sote tutaenenda **katika nuru ya Kristo,** ambayo ni **kuenenda katika upendo na haki**, twashirikiana naye na pia sisi kwa sisi. Ikiwa twaenenda mbali na nuru Yake, twatoa vivuli, twatenda dhambi na kupoteza furaha yetu na kuwasababishia matatizo walio karibu nasi na walio makanisani mwetu.

**4. Jifunze kushuhudia:** Tunahitajika tujifunze jinsi ya kushuhudia kwa wasio Wakristo na kuwaeleza kuhusu Bwana Yesu, na jinsi anavyowaokoa toka dhambini. **Jifunze kuwaeleza jinsi ulivyofanyika kuwa Mkristo, kwa kuwa huu ndio ushuhuda wako!** *"Bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu, lakini kwa upole na kwa hofu"* (1 Petro 3:15).

**T**unahitajika tulifahamu 'Neno' la Mungu, ili tuwe *"analishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima,na kuwashinda wenye kupinga"* (Tito 1:9).

**W**akristo wote wana jukumu la kuishi maisha yanayosifia Injili, na kutafuta fursa ya kuwaeleza wengine kuhusu wokovu ambao unapatikana katika Bwana wetu Yesu Kristo. Na haya ndio waumini wa Thesalonike walifanya: *"Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma."* Pia *"mlivyomgeukia Mungu*

*mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli, na kumngojea Mwanawe kutoka mbinguni"* (Ona 1 Wathesalonike 1:8-10).

## Kufunza Ubatizo na mambo yote

**B**wana Yesu aliwaamuru wanafunzi wake **wabatizwe.** Neno hilo lamaanisha **'kutumbukiza'** au **'kuzamisha'** na maji mengi yanahitajika kwa kusudi hili kwa sababu katika ubatizo twajitambulisha pamoja na Kristo katika kifo chake, kuzikwa na kufufuka, na kwa njia hiyo maisha mapya (Warumi Sura 6). Maji mengi yaanahitajika ili wabatize, yamaanisha **kuzamisha kabisa** (Yohana 3:23). Kuwanyunyizia watoto au watu wazima maji haipatikani katika Biblia.

**T**unaposoma kitabu cha Matendo ya Mitume, twaona kuwa **waumini wote** walibatizwa kwa kukiri kwao kwa imani: *"Wakawa wakienda njiani, wakafika mahali penye maji. Yule towashi akasema, "Tazama, maji haya. Ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema, "Ukiaminikwa moyo wako wote, inawezekana." Akajibu, aakanena, "Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu"* (Matendo ya Mitume 8:36-37).

**T**unafaa tubatize kwa **jina moja** la **Baba, Mwana na Roho Mtakatifu**. Hili latufunza ukweli wa **Utatu wa Uungu**. **Nafsi** tatu, bali **Mungu** mmoja. Tunasoma *'Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi'* (Mwanzo 1:1). Utatu ni fiche katika neno **'Mungu'** kutoka katika Kiebrania **'elohim'**. Neno hili ni neno la **wingi,** tena kurejelea ukweli huo. Tunaona tena maneno haya: *"Mungu akasema, "**Na tumfanye** mtu kwa **mfano wetu**, kwa **sura yetu"*** (Mwanzo.1:26). Yesu akasema, *"Aliyeniona mimi amemwona Baba"*. Pia twaona **utatu** katika ubatizo wa Bwana wetu, kwa maana **Roho wa Mungu** alishuka juu yake **Yesu, aliye Mwana,** kwa mfano wa hua, nayo sauti ya **Baba** ikasikika toka mbinguni (Mathayo 3:13-17).

**T**unafaa kuwafunza wanafunzi kile ambacho mitume waliwafunza waongofu wapya, *"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali"* (Matendo ya Mitume 2:42). Yesu akasema *"kuwafundisha kuyashikayote niliyowaamuru ninyi"* (Mathayo 28:20). Tunafaa kuwafunza wanafunzi:

**a.** Kuyafuata mafundisho ya mitume.

**b.** Kudumu katika ushirika na waumini wengine.

**c.** Kuendelea na Chakula cha Bwana

**d.** Kukusanyika kwa ajili ya kusali.

## Upanzi wa Kanisa

Bwana alilipanga kanisa (Mathayo Sura za 16 & 18). Anataka watu wake wawe wakikutana kila Siku ya Bwana (Jumapili, siku ya kwanza ya juma) kuendeleza mafundisho haya. Tunapowaongoza watu kwake Kristo, tunahitajika tuwakusanye wote pamoja katika jina la Bwana (Mathayo 18:20), na kuwaagiza katika mafundisho yote yaliyomo katika Biblia.

**Kumbuka, Yesu alisema,** *"...na tazama, mimi nipo **pamoja nanyi** siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* Atakuwa pamoja nasi siku zote, na tunapomtazama katika maombi, atafanya mapito mbele yetu kwa njia tunayofaa kuifuata.

**Bwana akusaidie na kukubariki unapoenenda katika nuru ya Neno lake.**

**-----------------------------------------------------**

**Sura 7**

# Nyumba ya Mungu

**Hili ni fundisho zito kwa makanisa la mahali. Wao ni sehemu ya mwili Wake, Kanisa la mbingu. Yote yaonekana hapa yakiwa wamechanganyika.**

**K**atika maandishi ya mtume Paulo, tunafunzwa jinsi Bwana anavyowathamini watu wake, na makanisa ya mahali ambapo wanakutana. *"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu **hekalu la Mungu**, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi"* (1 Wakorintho 3:16-17). Kanisa la mahali na miili yetu ni hekalu!

**N**i lazima tutunze mwenendo wetu katika nyumba Yake: *"Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli"* (1 Timotheo 3:14-16).

**B**wana Yesu yuko pamoja na watu wake wanapokutana: *"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao"* (Mathayo 18:20). Kanisa la mahali ni *"Kanisa la Mungu aliye Hai",* naye Yesu akiwa msimamizi miongoni mwa watu Wake, ambapo washirika wote imewapasa wawe na kicho na ibada.

**B**wana Yesu Kristo ndiye mmiliki wa nyumba hii. *"bali Kristo, kama mwana, juu ya nyumba ya Mungu, ambaye nyumba yake ni sisi"* (Waebrania 3:1-6).

**K**risto ndiye msingi wa mwili Wake, Kanisa: Ambayo *"ndiyo nguzo na msingi wa kweli"* (1 Timotheo 3:14-16). Ni 'nguzo' (tegemezo) na 'msingi' (shina) uliojengwa juu ya Kristo, kwa kuwa alisema *"nitalijenga kanisa Langu"* (Mathayo 16:13-19). *"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo"* (1 Wakorintho 3:11).

"*Na bila shaka **siri ya utauwa ni kuu:** Mungu alidhihirishwa katika mwili, Akajulika kuwa na haki katika Roho, Akaonekana na malaika, Akahubiriwa*

*katika mataifa, Akaaminiwa katika ulimwengu, Akachukuliwa juu katika utukufu"* (1 Timotheo 3:16).

**S**iri ya utendaji wa Mungu yaonekena: **a.** Kuzaliwa kwake na bikra, kwa maana *'alidhihirishwa katika mwili'*. **b.** Katika maisha Yake kamilifu, kwa maana *'Akajulika kuwa na haki katika Roho'* machoni pake Baba, mkamilifu, Mwanadamu asiye na dhambi aliyekufa msalabani kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. **c.** *'Akaonekana na malaika',* kwa maana walimhudumia (Mathayo 4:11). **d.** Wakati habari hii ya ajabu ilipohubiriwa ili *'aminiwa katika ulimwengu'.* **e.** Wanafunzi walimtazama wakati alipokuwa *'akichukuliwa juu katika utukufu'*

**'*Siri ya Utauwa'* ni Kristo aliyedhihirishwa katika mwili. Roho wake akiwa ndani yetu atuwezesha kuishi katika utauwa na kuonekana katika baisha yaliyobadilishwa.**

## Kuingia na ibada katika Nyumba Yake

**Kuna njia moja pekee ya kuingia:** Yesu alisema: *"Mimi ndimi mlango"* (Yohana 10:7-9). Imewapasa wote kuingia kupitia Yesu ili wawe sehemu ya jamaa Yake.

**Ni nyumba ya *'imani':*** *"Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema, hasa **jamaa ya waaminio**"* (Wagalatia 6:10). Twaingia katika jamaa Yake kwa imani ili tuokolewe na kupokea kipawa cha uzima wa milele (Yohana Sura 10). Ni nyumba ya kiroho iliyojawa na watu wa kiroho:

**a.** Wao ni ukuhani mtakatifu kwa sababu wametakaswa (wametengwa) na Roho Mtakatifu anayekaa ndani yao na kwa damu ya thamani isafishayo yake Yesu (1 Petro 2:1-5).

**b.** Wao ni ukuhani wa kifalme kwa sababu wamefanyika kuwa wana katika jamii ya Mfalme wa wafalme (1 Petro 2:9). Wao sasa ni wana wa Mungu kwa kuzaliwa upya (Yohana 1:11-13), na wana wa Mungu kwa kufanywa kuwa wana (Warumi 8:15-16).

**W**aumini wana uhusiano wa ajabu na Kristo: *"Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe **nyumba ya Roho**, **ukuhani mtakatifu**, mtoe **dhabihu za roho**, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo"* (1 Petro 2:4-5).

**W**ale wote wanaoamini wanaunda mwili wa Kristo: *"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa **nyumbani mwake Mungu**"* (Waefeso 2:19).

## Utakatifu wa nyumba Yake ni lazima ulindwe

**a.** Ni hekalu takatifu, maskani ya Mungu: *"Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana"* (Waefeso 2:21).

**b.** Utakatifu unapaswa kuwa alama ya wana wa Mungu: *"bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote, kwa maana imeandikwa, "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu"* (1 Petro 1:14-16).

"***Shuhuda zako ni amini sana; Utakatifu ndio uifaao nyumba yako, Ee BWANA, milele na milele"*** Zaburi 93:5

**M**wito wa kujitenga na vyombo vilivyo chafu: *"Basi katika **nyumba kubwa** havimo vyombo vya dhahabu na fedha tu, bali na vya mti, na vya udongo, vingine vina heshima, vingine havina. Basi ikiwa mtu amejitakasa kwa kujitenga na hao, atakuwa chombo cha kupata heshima, kilichosafishwa, kimfaacho Bwana, kimetengenezwa kwa kila kazi iliyo njema"* (2 Timotheo 2:19-21). Ni *'nyumba* kubwa' iliyo na vyombo safi na vichafu. Ni lazima tujitenge mbali na waumini ambao hutenda mambo yaliyo machafu.

**M**wito wake Mungu kwa watu Wake: *"Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana. Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.* (2 Wakorintho 6:17-18).

**Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu** (1 Wakorintho 6:19-20). Ni lazima tusiitie unajisi kwa uzinzi, uasherati au matendo mengine machafu. Ni lazima tuwe vyombo vilivyo safi ili tubebe Injili hadi nje kwa ulimwengu (Isaya 52:11).

**Sisi wale tunaoamini tunaubeba ujumbe na majukumu yaliyo na matokeo ya milele na thawabu za milele.**

## Kusudi la Nyumba Yake

**Ni nyumba ya sala -** *Akawaambia, "Imeandikwa, 'Nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala,' bali ninyi mmeifanya kuwa 'pango la wanyang'anyi.'"* (Mathayo 21:13).

Ni jambo la kuhuzunisha wakati ambapo kanisa la mahali linakosa kukutana kwa ajili ya sala, Chakula cha Bwana na mafundisho. Wakristo wa kwanza walikuwa waaminifu: *"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali"* (Matendo ya Mitume 2:42). Maandiko yaliyovuviwa yasema: *"wala tusiache kukusanyika pamoja, kaama ilivyo desturi ya wengine, bali tuonyane, na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia"* (Waebrania 10:25).

**Sala ni umuhimu wa 'kwanza' wa kitume: Mambo ya kuyaombea:** *"Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike*

*kwa ajili ya watu wote, kwa ajili ya wafalme na wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu"* (1 Timotheo 2:1-2).

**Kile ambacho Baba atafuta kutoka kwa nyumba Yake.**

"Waabuduo halisi watamwabudu Baba ***katika roho na kweli****; Kwa maana* ***Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu****"* (Yohana 4:23).

**Huu ndio wajibu wa kwanza wa waumini wa kweli, kwa hali zote, kibinafsi na kusanyiko, kumwabudu katika 'roho na kweli', na kuenenda katika utakatifu pamoja na Bwana wetu.**

## Kuhani Mkuu juu ya Nyumba ya Mungu

"*Na kuwa kuhani mkuu juu ya* ***nyumba ya Mungu****, na* ***tukaribie*** *wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali* ***tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya****,* ***tumeoshwa miili kwa maji safi****"* (Waebrania 10:21-22).

**Twafurahi kwa sababu ya kile ambacho Kristo alitutendea pale Kalvari:** *"Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye,* ***maana yu hai siku zote ili awaombee****"* (Waebrania 7:25). **Kuhani wetu Mkuu ameketi juu mbinguni naye anatuombea, ili atutimizie kila hitaji.**

'**Nyumba ya Mungu' iliytokamilika:** Siku moja hivi karibuni, 'Nyumba ya Mungu' kama kanisa la mahali haitakuwepo: bali Kanisa ambalo ni mwili Wake litakuwa limekamilika, na kuwasilishwa kwake Kristo kama bibi arusi wake aliye mkamilifu (Waefeso 5:25-27).

"***Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake, kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari."*** (Ufunuo 19:7).

**------------------------------------------------------**

**Sura 8**

# Kuja kwa Bwana

**K**uja kwa Bwana kwa ajili ya watu wake ni mojawapo ya matukio ya ajabu zaidi yaliyoahidiwa katika Neno la Mungu. Litatokea ghafla, nalo litatukaribisha katika utukufu wa uwepo Wake. Tupaswa tuwe tunaishi kwa ajili ya hili na kulitazamia wakati wowote ule. Yapasa kutujaza na bidii ya kumtumikia Yeye kwa uaminifu.

**Tunapaswa tuwe:** *"tukilitazamia* ***tumaini lenye baraka*** *na* ***mafunuo ya utukufu*** *wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu, ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema"* (Tito 2:13-14).

**Tunapaswa kuishi kwa ajili ya mbinguni:** *"Kwa maana sisi,* ***wenyeji*** *wetu* ***uko mbinguni****, kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo,* ***atakayeubadili*** *mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na* ***mwili wake wa utukufu****, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake"* (Wafilipi 3:20-21).

**Tutafanana Naye:** *"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa, lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye"* (1 Yohana 3:2).

## Yuaja <u>kuwachukua</u> watu Wake

**Haya yalifunzwa na Bwana Yesu:** *"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia. Maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali,* ***nitakuja tena niwakaribishe kwangu****; ili nilipo mimi, nanyi mwepo"* (Yohana 14:1-3).

**Mtume Paulo pia alifunza haya:** *"Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa* ***neno la Bwana****, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika* ***hatutawatangulia*** *wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu* ***Bwana mwenyewe*** *atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu. Nao* ***waliokufa*** *katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia,* ***tutanyakuliwa*** *pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani. Na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele"* (1 Wathesalonike 4:14-17).

**Soma pia 1 Wakorintho Sura 15.** *"Angalieni, nawaambia ninyi siri: hatutalala sote, lakini sote tutabadilika,* ***kwa dakika moja****, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho. Maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika"* (1 Wakorintho 15:51-52).

**Kutoka hapa twajifunza:** Wakati wakristo wanapokufa, miili yao huenda mavumbini, bali nafsi na roho zao kwa mara moja ziko na Bwana zikifurahia uwepo Wake (2 Wakorintho 5:8). Wakati Bwana atakaporejea, waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza, waumini walio hai **watanyakuliwa** (kuchukuliwa kimwili) pamoja nao kukutana Naye **mawinguni.** Nasi tutakapomwona tutabadilishwa na tutafanana Naye na kuwa Naye milele.

## Atawahukumu watu Wake

**B**aada ya **'unyakuo'** tutaenda hadi kwenye ***'kiti cha hukumu cha Kristo'*** kwa ajili ya **'kuchunguzwa'** na **'kupewa thawabu'.** Kwa maana imetupasa sisi sote kusimama mbele ya Bwana wetu, **sio kwa ajili ya dhambi zetu**, bali kwa ajili ya **kuyachunguza** matendo yetu yaliyotendwa katika mwili; hiyo ni kwa ajili

ya utumishi wetu, kilichotuchochea na nia zetu, iwapo ni **mema au mbaya.** Kisha atawapa **thawabu** watu Wake, kwa sababu kuna **taji** zitakazotuzwa iwapo tumemfuata Bwana kwa uaminifu.

**Biblia yasema:** *"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"* (Soma 2 Wakorintho 5:6-11).

**H**ii siyo hukumu ya dhambi zetu, kwa maana Kristo alilipa deni hilo Kalvari. Yesu alisema: *"Amin, amin, nawaambia, yeye alisikiaye neno langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele, wala **haingii hukumuni**, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani"* (Yohana 5:24).

**W**atu wake wataandaliwa kwa ajili ya **kushangilia** katika arusi ya Mwana-Kondoo (Ufunuo 19:7-10). kwa sababu hiyo, mtume Paulo aliutumikisha mwili wake, ili asije **'akakataliwa'.** Kwa kuzingatia hili, mtume Paulo anautesa mwili wake ili asije akawa **'mtu wa kukataliwa'.** Hii inamaanisha kuupoteza **ushuhuda wake wa sasa** na **thawabu ya siku ijayo** (1 Wakorintho 9:24-27).

## Kuja kwake pamoja na watu Wake

**B**wana atarejea duniani **pamoja** na watu Wake, ili **auhukumu** ulimwengu katika haki na kuuleta ufalme wake duniani (Ufunuo 19:11-21, Sura 20). Na siku hiyo **miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki.** Kwa ajili ya toba ya Israeli na matukio ya kutikisa nchi ya Siku hio, soma Zekaria Sura 12 hado 14.

**H**iyo 'Siku ya Bwana' ya kutisha imetajwa katika Maandiko mengi (Soma Yoeli 2:31-32), *"kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua. Naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu"* (Matendo ya Mitume 17:31).

**Atakapowajia watu wake, tutakutana naye mawinguni.**

**Atakapokuja pamoja na watu wake, miguu yake itasimama juu ya Mlima wa Mizeituni katika Yerusalemu.**

## Kuyarejelea haya matukio

Bwana Yesu Kristo aliwafundisha wanafunzi wake kuhusu **kuwajilia mawinguni** (Yohana 14:1-3). Wakati wowote tunaposhiriki Chakula cha Bwana, *"mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo"* (1 Wakorintho 11:26). Kanisa linapaswa kumngojea Bwana Yesu arejee wakati wowote (1 Wathesalonike 1:9-10) baadaye dhiki kuu itakayodumu miaka saba, inayoitwa wakati wa taabu yake Yakobo au Israeli. (Ona Yeremia Sura 30; Danieli 9:24-27; Mathayo Sura 24; Ufunuo 7:13-14). Waumini watakua mbinguni kwenye kiti cha hukumu cha Kristo.

Kisha Bwana atarejea **pamoja na watakatifu wake duniani** kwa nguvu na utukufu mwingi na kuuanzisha utawala wake wa miaka 1,000 (Milenia). Ufufuo na hukumu ya waovu itafuata, na kisha hali ya umilele (Soma Ufunuo Sura 19 hadi 22).

Pia Bwana wetu Yesu aliwafunza wanafunzi wake kuzitumia karama zao alizowapa, na kuwaambia *"Fanyeni biashara hata nitakapokuja"* (Luka 19:13). Baadhi ya mifano Yake iliwafunza wanafunzi wake kuwa tayari kwa kudhihirishwa kwake wakati wowote.

**Acheni tuwe na shughuli tukimtumikia Bwana, tukikutana na watu wake na kungojea kuja kwake.**

**---------------------------------------------------**

# Utu na Kazi ya

# Roho Mtakatifu

Somo na Albert Fairweather

**Maswali yajibiwa kuhusu:**

**Ubatizo wa Roho Mtakatifu**

**Kutoa Unabii, Kunena kwa Lugha & Uponyaji**



***"Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele"* John 14:15-16**

## Utu na Kazi ya Roho Mtakatifu

**K**una kuchanganyikiwa kwingi hivi leo kuhusu Utu na kazi ya Roho Mtakatifu. Maswali huibuka kuhusu **"Roho Mtakatifu ni nani", "Ubatizo wa Roho Mtakatifu", "Kutoa unabii", "Kunena kwa Ndimi"** na **"Uponyaji".**

**B**wana Yesu Kristo aliwafundisha wanafunzi wake kuhusu kuja na huduma ya Roho Mtakatifu: *"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui, bali ninyi mnamtambua, maana anakaa **kwenu**, naye atakuwa **ndani yenu**. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu"* (Yohana 14:16-18).

**P**ia akasema kuwa Roho Mtakatifu: *"atawafundisha yote"* (Yohana 14:26); *"Atanishuhudia"* (Yohana 15:26); Ata *"uhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu"; "mambo yajayo atawapasha habari yake"* na *"atanitukuza mimi"* (Yohana 16:7-15). Kutoka kwa haya twajifunza:

**1.** Kwa kuyajibu maombi ya Bwna Yesu, Roho Mtakatifu angepelekwa na Baba. Anaitwa 'Msaidizi' au 'Mfariji'.

**2.** 'Yeye' ni Nafsi, wala sio nguvu, kwa maana Yeye ni *"Roho wa kweli"*. ambaye ulimwengu hauwezi kumtambua, kumwona wala kumpokea.

**3.** Wanafunzi wangemtambua, kwa maana Alikuwa **'pamoja'** nao kama vile Yesu alivyosema, na kisha baadaye angekuwa **'ndani'** yao naye *'atakaa nanyi hata milele'*.

**4.** Angekuwa na huduma kwa ulimwengu, kuwahakikisha kwa habari ya dhambi, na haki na hukumu.

**5.** Angekuwa na huduma kwa waumini, kuwafunza na kumtukuza Kristo.

## Baba, Mwana na Roho Mtakatifu

**I**ngawa neno **'Utatu'** halionekani kamwe katika Biblia, fundisho hilo liko. Ona kile Bwana Yesu Kristo alichosema: *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa **jina** la **Baba,** na **Mwana,** na **Roho Mtakatifu,** na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" Amina"* (Mathayo 28:18-20). Ubatizo unafaa ufanywe kwa **jina moja,** lakini ni **nafsi tatu** za Uungu zimetajwa katika umoja huu.

'**Utatu'** pia waonekana katika ubatizo wa **Bwana** – **Roho wa Mungu** alishuka kama hua na kukaa juu ya **Mwana**, na sauti ya **Baba** ikasikika kutoka mbinguni (Mathayo 3:13-17).

'**Utatu'** pia waonekana katika Waebrania 9:14, wote wakitenda kazi pamoja kutuletea ukombozi: *"basi si zaidi damu yake **Kristo**, ambaye kwamba kwa*

***Roho wa milele** alijitoa nafsi yake kwa **Mungu** kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?”*

**B**iblia yafunza wazi Uungu wa Bwana Yesu Kristo na Roho Mtakatifu, na ya kuwa Baba aliwapeleka wote ulimwenguni! *“Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu”* (1 Yohana 4:14). *“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele” “kutoka kwa Baba”* (Yohana 14:16; 15:26).

## Roho Mtakatifu ni Mungu na Bwana

**P**etro pia alielewa Uungu wa Roho Mtakatifu: *“Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo **Roho Mtakatifu** ...Hukumwambia uongo mwanadamu, bali **Mungu**”* (Matendo ya Mitume 5:1-4). Anaitwa: *“Roho wa milele”* (Waebrania 9:14); *“Roho wa uzima”* (Warumi 8:2) na *“Roho wa kweli”* (Yohana 14:15-17) na mengine mengi. Hizi zote ni sifa za Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

**Ana utu, kwa maana awezadanganywa, huzunishwa na kuzimishwa.**

**B**iblia yafunza wazi kuwa Roho Mtakatifu ni mmoja na Baba na Mwana. *“Basi **Bwana ndiye Roho**; walakini alipo **Roho wa Bwana**, hapo ndipo penye uhuru”* (2 Wakorintho 3:17).

## Yesu Kristo pia ni Mungu na Bwana

**T**okea nyakati za zamani Wakristo walielewa kuwa **Bwana Yesu ni *‘Mungu aliyedhihirishwa katika mwili’*** (1 Timotheo 3:16): *“Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa Mwana, nao watamwita jina lake **Imanueli**, yaani “**Mungu pamoja nasi**”* (Mathayo 1:23; Isaya 7:14). Anaitwa *“Bwana Yesu Kristo”* zaidi ya mara 80 katika Agano Jipya. Neno ‘Bwana’ latueleza kuwa Yeye ni Mungu: *“Tomaso akajibu, akamwambia, **Bwana** wangu na **Mungu** wangu!”* (Yohana 20:28).

**Z**aidi ya miaka 700 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, Isaya aliandika: *“Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake. Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, **Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele**, Mfalme wa amani”* (Isaya 9:6).

**Kutokana na hayo tunaona kuwa kuna Nafsi tatu katika Uungu, bali wao ni mmoja katika asili.**

## Kupelekwa kwa Roho Mtakatifu

**N**i muhimu kutambua kuwa Roho Mtakatifu hakupelekwa hadi Bwana Yesu atukuzwe: *“Na neno hilo alilisema* (Yesu) *katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; **kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa**”* (Yohana 7:39). Baada ya kufa na kuzikwa, alifufuka tena siku ya tatu na akawa akiwafundisha wanafunzi kwa muda wa siku 40, na kisha akapaa kutoka machoni pao na akatukuzwa juu mbinguni (soma Matendo ya Mitume Sura 1). Kisha akamwomba Baba, naye Roho Mtakatifu akapelekwa kutoka mbinguni sikukuu ya Pentekoste, siku 50 baada ya kufufuka kwake (Matendo ya Mitume Sura 2). Kanisa (jambo jipya) likaundwa, kwa kuwa Bwana Yesu alisema *“juu ya mwamba huu **nitalijenga** kanisa langu”* (Mathayo 16:18). **Ona:** Ilikuwa bado ni wakati ujao alipoyasema maneno hayo.

**Y**ohana Mbatizaji alitabiri kupelekwa kwa Roho Mtakatifu. *“Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba, bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake, yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto”* (Mathayo 3:11).

**B**wana Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake ahadi hii (Luka 24:49; Matendo ya Mitume 1:4-5) ambayo ilitimizwa siku ya Pentekoste: *“Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao”* (Matendo ya Mitume 2:1-3).

**H**ii ndiyo iliyokuwa siku ya kuzaliwa ya Kanisa, **tukio la mara moja pekee, lisirudiwe tena.** Kuna **ubatizo mmoja** pekee, *“Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote ndani ya yote”* (Waefeso 4:4-6).

**Kwa kujibu ombi la Kristo, Baba alimpeleka Roho Mtakatifu aliyewabatiza wanafunzi katika mwili mmoja, Kanisa!**

## Ubatizo wa Roho

**N**i makosa kufundisha “Ubatizo wa Roho Mtakatifu” au kusema kuwa waumini wabatizwe **katika** ama **ndani** ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ndiye **‘mbatizaji’** ambaye siku ya Pentekoste **‘aliwabatiza’** wanafunzi **katika mwili mmoja**, *“Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani, ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja”* (1 Wakorintho 12:13).

**K**atika Kigiriki, *“sisi sote tumebatizwa”* ipo **katika wakati uliopita na imekamilika** – tukio ambalo haliwezirudiwa! Kanisa ndilo huu **‘mwili’** unaojumlisha waumini toka siku ya Pentekoste ulipoundwa, hadi siku Bwana Yesu atakapowachukua watu wake kwenda nyumbani mbinguni (Yohana 14:1-3).

**W**akati wa kuongoka. Kila muumini hupokea mema haya, na kuwa sehemu ya mwili wa Kristo, na mshirika wa Kanisa lake. Hili ni jambo ambalo Roho Mtakatifu hutufanyia, nalo liko mbali na ‘uzoefu’ wowote.

**B**wana Yesu alimwambia Petro kuwa atampa *“funguo za ufalme wa mbinguni”* (Mathayo 16:18-19). Funguo hutumika kufungua milango, naye Petro alitumika

kufungua milango ya ufalme wa mbinguni, kwanza kwa Wayahudi (Matendo ya Mitume 2:14-47); tena kwa Wasamaria (Matendo ya Mitume 8:14-17); kisha kwa Wayunani (Matendo ya Mitume 10:1-48).

**K**atika haya yote tunaona jinsi Bwana alivyokuwa akiuendeleza ufalme wa mbinguni katika maeneo mapya, kama mji ambao una ugavi wa maji uliounganishwa kwa kila kitongoji unavyozidi kukua. Mwishowe, Paulo (mtume pia) alitumika kuendeleza ufalme kwa wanafunzi wa Yohana Mbatizaji (Matendo ya Mitume 19:1-7). Watu hawa hawakuwa wamesikia kuhusu Roho Mtakatifu na walifahamu machache kuhusu Bwana Yesu. Walijua ubatizo wa Yohana wa toba kwa ajili ya msamaha wa dhambi.

**K**atika utaratibu wa Mungu ilikuwa Wayahudi kwanza, mahali ambapo mwili, Kanisa lilianza. Kisha kukawa na kuendelea hadi kwa Wasamaria mahali ambapo vizuizi vya **kidini** viliondolewa. Kisha kwa Wayunani ambapo vizuizi vya ubaguzi wa jamii viliondolewa. Na mwishowe vizuizi vya vipindi vikaondolewa wakati wanafunzi wa Yohana Mbatizaji waliletwa kutoka kipindi cha torati hadi cha Kanisa la Agano Jipya.

**S**asa katika haya kipindi cha Kanisa, kipindi cha neema, wale wote wanaoamini wanabatizwa na Roho mmoja katika mwili mmoja. Ni umoja wa ajabu vipi huu, unaoondoa vizuizi vyote vya kidini, jamii na vipindi! Kweli kuna ***"mwili mmoja"*** pekee (Waefeso 4:5).

## Kujazwa na Roho Mtakatifu

**R**oho Mtakatifu ndiye **'Msaidizi'** au **'Mfariji'**, yamaanisha **'anayekaribia kando ili kusaidia'**. Angepelekwa ili kuwasaidia wanafunzi katika hali zote za maisha yao. Wakati Bwana Yesu alipokuwa na wanafunzi, alikuwa Msaidizi na Mfariji wao! Hangewaacha yatima; angewajilia katika utu wake Roho Mtakatifu ambaye angechukua nafasi Yake hapa duniani (Yohana 14:15-18).

**N**i vibaya kuzungumzia baraka ya pili, jambo fulani 'lisilo la kawaida' linatendeka baada ya kuongoka. Hapa watu wanachanganya **ubatizo wa Roho** katika mwili mmoja, na **kujazwa na Roho Mtakatifu.** Kuna "ubatizo mmoja" pekee. Biblia yasema, *"Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu; Bwana mmoja, imani moja, **ubatizo mmoja;** Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote"* (Waefeso 4:4-6).

**Kuna kujazwa kwingi kwa Roho Mtakatifu.** Baada ya Roho Mtakatifu kupelekwa na mwili mmoja, Kanisa, ukaundwa, wanafunzi walijazwa na Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 2:4; 4:8, 31; 9:17).

**K**uombea au kutarajia 'Ubatizo wa Roho' mwingine hakujatajwa popote katika Biblia, **bali kujazwa na Roho Mtakatifu kumetajwa mara kwa mara.** Biblia yatueleza kuhusu kujazwa huku: *"Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali **mjazwe Roho**"* (Waefeso 5:18). Katika lugha ya Kigiriki hii ni **amri ya kuendelea kujazwa.**

**M**tu aliyelewa mvinyo yuko chini ya ushawishi wa roho wa mvinyo, na hivyo anatenda kipumbavu. Tofauti na hilo, mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu hutenda tofauti, akionyesha ushawishi na tunda la Roho Mtakatifu katika maisha yake. *"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi. Juu ya mambo kama hayo hakuna sheria"* (Wagalatia 5:22-23).

**T**umeamriwa *"tujazwe Roho"* (Waefeso 5.18), *"tuenende kwa Roho"* (Wagalatia 5:16). *"tuongozwe na Roho"* (Wagalatia 5:18), na kudhihirisha *"tunda la Roho"* maishani mwetu.

## Kuenenda kwa Roho

**B**iblia pia yasema: *"**Tukiishi** kwa Roho, na **tuenende** kwa Roho"* (Wagalatia 5:25). Kila muumini **yuaishi katika nyanja** ya Roho Mtakatifu kwa njia ya kuzaliwa upya na kwa kubatizwa na Roho Mtakatifu katika mwili wa Kristo.

**S**asa twaambiwa **tuenende** katika Roho, kwa maana **tunawezamhuzunisha** na **kumzimisha** Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu. *"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi"* (Waefeso 4:30). *"Msimzimishe Roho"* (1 Wathesalonike 5:19).

**T**unapokosa kutii, kufanya chaguzi mbaya, kuishi maisha ya ubinafsi au dhambi, **tunamhuzunisha** au kumuumiza Roho Mtakatifu na **kuuzimisha** moto ambao anaoangaza nao mioyoni mwetu ili tumtumikie na kuishi kwa ajili yake. Hatutakuwa na amani na furaha ambayo mfuasi wa kweli wake Kristo anapaswa kuwa nayo. Yeye ni **'Roho Mtakatifu'**, naye hufanya kazi ya kuzalisha **utakatifu** katika maisha yetu. Tukiendelea kutenda dhambi, hatakuwa na uwezo wa kututumia, kwa maana anataka vyombo safi katika utumishi wake.

**H**atupaswi kutafuta **ubatizo wa Roho**, bali tunapaswa kutafuta **kujazwa na Roho**. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni **kazi ya Mungu ndani yetu wakati wa kuongoka**; kujazwa **kujitoa kwetu kwa mapenzi ya Mungu maishani mwetu**, ni hitaji la siku baada ya siku.

## Kujitoa kwa Roho Mtakatifu

**R**oho Mtakatifu anataka **kumiliki** kila chumba ndani ya mioyo yetu. Mara kwa mara kuna vyumba ambavyo hajakaribishwa! Vyumba hivi vinawezakuwa vinamilikiwa na mawazo mabaya na ya dhambi, roho ya kutosamehe, au malengo ya kidunia na matendo ya dhambi. Hatuwezi jua furaha na amani kamili hadi tuyatoe yote kwake. *"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu"* (1 Wakorintho 6:19-20).

**P**aulo aliwaandikia Wakristo wa kimwili au kidunia maneno haya (1 Wakorintho 3:1-3). Kanisa hili liliwakubali na baadhi yao walikuwa wanayatenda mambo ya dhambi. Hawakuwa wamejazwa na Roho. Wakati wowote tunapojipata tukiyatenda mambo yanayomhuzunisha Yeye. Tunahitajika tuungame na kuyaacha mambo hayo: *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote"* (1 Yohana 1:9).

**Sasa ndio wakati wa kufurahia kujazwa huku kwa kuyatoa yote kwake. Yeye ana kazi maalum kwa kila mmoja kufanya, na kuna furaha na amani katika kuishi kwa ajili ya Bwana na kutumika Naye anapoendeleza ufalme wake miongoni mwa watu leo.**

## Kazi ya Roho Mtakatifu 'kwa ajili' na 'ndani' Yetu

**U**batizo wa maji waweka wazi uhusiano wa ajabu kati yetu na Kristo na msimamo wetu kama tumefichwa ndani Yake: *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima"* (Warumi 6:1-14).

**K**upitia kwa kazi ya Roho Mtakatifu, tumetambulika pamoja na Kristo, ili kwamba Paulo aweza sema: *"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu, na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu"* (Wagalatia 2:20).

**P**ia Paulo akaandika, *"Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu"* (Wakolosai 3:1-4).

**H**ivi ndivyo Mungu aonavyo kila muumini: Wakati Kristo alipokufa, tulikufa pamoja naye; alipozikwa, tulizikwa pamoja naye, na alipofufuka, tulifufuka pamoja naye. Ona jukumu la muhimu la Roho Mtakatifu katika haya:

**1.** Tulihakikishiwa kwa habari za dhambi na Roho Mtakatifu na kuletwa kwenye toba na imani (Yohana 16:8-11).

**2.** Tulizaliwa mara ya pili *"kwa maji na kwa Roho"* na kufanyika wana wa Mungu (Yohana 1:11-13; 3:5).

**3.** Tulifanywa kuwa wana wa Mungu naye *"Roho ya kufanywa wana"* (Warumi 8:12-17).

**4.** *"Katika Roho mmoja... tulibatizwa kuwa mwili mmoja"*, Kanisa (1 Wakorintho 12:13).

**5.** *"Tumetiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu"* ishara ya usalama na kumilikiwa (Waefeso 1:13-14).

**6.** *"Tumetakaswana Roho Mtakatifu"* hii yamaanisha 'kutengwa' kwa ajili ya makusudi ya Mungu (Warumi 15:16).

**H**ii ni **nyanja ya Roho** ambamo twakaa ndani yake machoni pake Mungu! Kiumilele tumetambulika pamoja na Kristo machoni pa Baba kupitia kazi ya Kristo juu ya msalaba, na kupitia kwa Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu. Mungu ametufanyia mambo mengi ya ajabu nasi hatuwezi kuyaelewa yote kikamilifu kwa sasa. Tutamsifu na kumwabudu daima kwa jinsi alivyo na kwa yale amefanya katika umilele unaokuja.

## Roho Mtakatifu katika Agano la Kale na Karama Zake

**K**atika Agano la Kale Roho Mtakatifu alikuwa **'pamoja'** na watu wa Mungu na alikuja **'juu'** ya walioteuliwa ili kuwawezesha kumtumikia Mungu katika njia maalum (Waamuzi 14:6; 15:14; 1 Samweli 10:6-10). Alikuja juu ya Daudi, bali alimwacha Sauli (Waamuzi 16:20; 1 Samweli 16:13-14).

**D**audi akawa mfalme mkuu, nabii na mtunga zaburi mwema wa Israeli kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Baada ya dhambi yake kuu na Bathsheba, alitambua pia yupo katika hatari ya kuachwa na Roho Mtakatifu. Toba yake imenakiliwa katika Zaburi 51:11. Akamwomba Mungu, *"wala Roho yako Mtakatifu usiniondolee"*.

**D**audi alipoteza furaha ya wokovu wake (Zaburi 51:12) na alikuwa katika hatari ya kupoteza uwezeshwaji wa kuwa mfalme mwenye hekima na mwema , kuwa nabii na mwandishi wa Zaburi zilizovuviwa. Hizi zote zilikuwa ni **karama** kutoka kwa Roho Mtakatifu.

**H**ivi leo, Roho Mtakatifu hawezi kumwacha mtoto wa kweli wa Mungu, *"Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto* (haziwezi badilika), *wala mwito wake"* (Warumi 11:29). Nasi pia tuna ahadi ya ajabu yake Bwana Yesu Kristo: *"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, **ili akae nanyi hata milele**"* (Yohana 14:16).

**K**ila Mkristo amepokea karama, aliyopewa na Bwana aliyepaa (Waefeso 4:7-16) na Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 12:1-31). tunahitajika kumwomba Bwana atuonyeshe karama zetu ni zipi, na kisha tuzitumie kwa utukufu wake.

## Enzi za Mitume na Manabii kuisha

**P**aulo alifahamu kuwa hivi karibuni mitume na manabii wangekufa, na kwa hiyo Mungu akamfunulia ukweli huu: *"Upendo haupungui neno wakati wowote. **Bali ukiwapo unabii utabatilika**; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo **maarifa**, yatabatilika. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu, na tunafanya unabii kwa sehemu. Lakini ijapoile iliyo **kamili**, iliyo kwa sehemu itabatilika"* (1 Wakorintho 13:8-10).

**N**eno **'kamili'** lamaanisha **'kumalizika'**, na katika Kigiriki sio **'mtu'**, bali ni **'jambo'! Biblia** ndio jambo pekee duniani lililo **'malizika' na 'kamili'. H**akuna neno lakuongezwa wala kupunguzwa kutoka kwa kurasa zake (Ufunuo 22:18-19). Ndani yake kuna *"imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu"* (Yuda 3).

'**Maarifa'** ulikuwa ni uwezo ambao baadhi ya watu waliwezeshwa kukumbuka na kufunza mafundisho yaliyofunzwa na mitume na manabii. Maarifa haya yalikuwa ni kwa sehemu tu na kwa hivi sasa yanapatikana katika Biblia zetu.

**M**itume na manabii walikuwa ni wa kipindi cha msingi wa Kanisa na hakuna mahali popote tunaelezwa tuwateuwe mitume na manabii zaidi (Waefeso 2:19-20; 1 Wakorintho 3:10-11). Wao pamoja na karama zao maalum za miujiza, uponyaji na lugha hawako pamoja nasi kwani tuna Biblia iliyo kamilika.

**K**arama hizi hazihitajiki leo kwa ajili ya utendaji kazi wa kanisa la mahali. Zilikuwa ni za muda katika asili yake, zikatumika na Mungu kuwafanya watu waamini ujumbe wa mitume. Zilitajwa kwa muhtasari katika 1 Wakorintho Sura 12; zingebatilika katika 1 Wakorintho Sura 13 na kuzuiliwa kabisa katika matumizi yake katika 1 Wakorintho Sura 14. Ilimbidi Paulo arekebishe mengi ya matumizi mabaya na kuzuia matumizi ya karama hizi na waumini wa kimwili katika kanisa la Korintho.

**O**na **utaratibu** wa kimungu unaotolewa kwa ajili ya karama hizi: *"Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, **wa kwanza** mitume, **wa pili** manabii, **wa tatu** waalimu, kisha miujiza, **kisha** karama za kuponya waginjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha. Je! Wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri? Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora"* (1 Wakorintho 12:28-31).

**Mitume na manabii walikuwa wa kwanza katika utaratibu, lugha zilikuwa za mwisho, na sio wote waliokuwa na karama hizi.**

-------------------------------------------------------------------

# Je, Lugha ni za Leo?

**Kufundisha kuwa ikiwa mtu yeyote haneni kwa lugha yamaanisha hana Roho Mtakatifu ni kosa zito.**

**P**etro na wanafunzi walinena kwa 'ndimi' au 'lugha zinazofahamika' katika siku ya Pentekoste (Matendo ya Mitume 2:1-12). Watu waliokuwepo walikuja kutoka nchi tofauti pamoja na lugha tofauti; **kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe** matendo makuu ya Mungu. Paulo alinena kwa lugha zaidi ya wote, lakini hakunena katika mikutano ya kanisa (1 Wakorintho 14:18-19). Mungu alimpa karama hii ili aweze kuhubiri Injili kwa watu wote aliokutana nao katika nchi nyingi.

'**Lugha'** za leo hazitumiki kwa makusudi hayo na hazifanani na zile za kanisa la mapema. Lugha zilikoma pamoja na unabii na maarifa. Maarifa ni uwezo wa kukumbuka na kufundisha mafundisho ya mitume bila kuwa na Biblia (1 Wakorintho 13:8). Hivi leo wamishonari, hata wale wanaokiri kunena kwa lugha, wanajifunza lugha za watu wanaoenda kuwafanyia uinjilisti! Vinginevyo, ni lazima wawe na mtu fulani ili atafsiri.

**L**ugha zilikoma kufikia mwisho wa enzi ya mitume (96BK) na kwa wale walioishi muda mrefu zaidi ya wakati huo. Yohana Chrysostom (345BK-407BK) aliandika katika *'Hotuba'* ya *"ukomo kwa matukio yaliyokuwa ya kawaida siku hizo* (za mitume) *lakini hazijulikani siku zetu"*. Alisema *"zilikoma muda mrefu uliopita"* (*Hotuba 4*). Vuguvugu la sasa la dini za karama lilianza mwanzo wa 1900, wakati jaribio lilifanywa la kuzifufua karama hizi.

**W**engi wanafundisha kuwa ili upokee karama ya lugha, ni lazima uanze kwa kumsifu Mungu haraka iwezekanavyo, pumzika, acha akili iwe tupu, kisha anza kunena maneno yasiyoeleweka. Kisha Roho Mtakatifu atakuja juu yako nawe utapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu! Baadhi yao hubingiria kwenye sakafu, wakipiga yowe na kufanya mambo mengine ya ajabu. Hakuna mahali popote Biblia yafunza mambo kama hayo, tunapaswa kujua kuwa Shetani ni mdanganyifu. Wanawake pia hushiriki katika mikutano hii, ingawaje Biblia yasema *"wanawake na wanyamaze katika kanisa"* (ona 1 Wakorintho 14:31-34). Kutoka zamani za kale wanawake wamekuwa maarufu katika desturi za kipagani ambapo wananena matamshi ya kiajabu. Ikiwa Neno la Mungu litafunzwa kwa uaminifu, mambo haya ya ajabu yatatoweka.

**Biblia** yafundisha kuwa **'kiasi'** ni tunda la Roho (Wagalatia 5:23): *"Na roho za manabii huwatii manabii. **Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani, vile vile ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu**"* (1 Wakorintho 14:32-33). Wale wanaohubiri wanapaswa kuwa waangalifu wasisisimke kupita kiasi kwa kunena haraka, kupaza sauti na kuwachochea watu kuwa wenye kichaa. Manabii wa Baali waliopagawa na mapepo walitenda hivi, bali Eliya alitenda kwa utulivu pamoja na sala fupi (1 Wafalme 18:20-40). *"Sauti ndogo ya utulivu"* yake Mungu haikusikika katika upepo mwingi wa nguvu, tetemeko la nchi au moto (1 Wafalme 19:11-12).

**Mungu husikika wakati tunapomngojea kwa utulivu na kwa sala, nazo nafsi zinaokolewa tunapolihubiri Neno la Mungu kwa utulivu, kwa kicho na unyoofu.**

## Je Vipi Kuhusu Uponyaji?

**P**etro na Paulo waliwaponya watu, lakini sio katika kila wakati: *"Trofimo nalimwacha huko Mileto, hawezi"* (2 Timotheo 4:20). Kwa Timotheo akamwandikia: *"Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara"* (1 Timotheo 5:23). Kwanini hakuwaponya? Paulo alikuwa na *"karama za uponyaji"*, bali hata juu ya karama hizi zisizo za kawaida Mungu alikuwa Mwenye Enzi. Hawezi kuamuliwa au kuhadaiwa. Yeye hufanya kila kitu kulingana na mapenzi ya Enzi Kuu.

**L**eo hatuna mitume, manabii, au karama za lugha, unabii na uponyaji. Hata hivyo, tunajua na kuamini kuwa miujiza na uponyaji hutukia wakati mwingine hata leo **kwa kujibu sala na kama inavyompendeza Bwana.**

**I**kiwa yeyote angekuwa na *"karama za uponyaji"* leo, hospitali zingebakia tupu na wafu wangefufuliwa. Hii ndiyo changamoto kwa wale wanaokiri kuwa na karama hizi. Wakati Bwana Yesu alipokuwa hapa duniani, aliwaponya kikamilifu na kabisa wale wote waliokuja kwake, aliwafufua watu watatu kutoka kwa wafu, na kusababisha furaha kuu miongoni mwa umati. Wakati mwingine mitume nao pia walifanya hivyo, bali sio wakati wote.

### Kwa Kumalizia

**K**atika kufunza kuhusu karama hizi, Paulo aliyasema haya: *"Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora"* (1 Wakorintho 12:31). Alitufunza kuwa tunapaswa *"ufuateni upendo"* na *"lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu"*, kwa maana *"yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo"* (1 Wakorintho 14:1-3).

**U**pendo ndio jambo la muhimu, kwa maana upendo waunganisha, bali mabishano kuhusu karama hizi maalum walizopewa mitume na wanafunzi wa hapo awali yamegawanya makanisa mengi. Leo mwalimu amechukua nafasi ya nabii, na mafundisho yake yanapaswa kuwa ya:

**1. 'Kujenga'**, yaani 'kuwaelimisha' waumini katika imani yao takatifu.

**2. 'Kuhimiza'**, yaani 'kuwachochea' waumini kuwa watiifu na kuishi maisha yenye nidhamu.

**3. 'Kufariji'**, yaani 'kuponya' nafsi zilizo umia na mioyo iliyovunjika na kuwahudumia faraja.

**Na hebu tuwe waangalifu tusije tukapotoshwa kwa madai ya kusisimua kuhusu karama za ishara zisizo za kawaida, bali heri tujitoe kwa *"njia iliyo bora"* ya kupenda, kutunza na kusitawishana mmoja kwa mwingine katika mwenendo wa Kikristo.**

---

**If helpful print this page on the inside of the back cover?**